# USAWIRI WA MALEZI UNAVYOATHIRI UTAMBULISHO WA VIJANA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI.

**NA**

**JULITA A. WANJALA**

**Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili ya sanaa katika Chuo kikuu cha Nairobi.**

**OKTOBA 2015**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili wa sanaa katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi………………………………………
Tarehe……………………………………..
JULITA .A. WANJALA

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama washauri na wasimamizi tulioteuliwa na chuo.

Sahihi……………………………………… ………………………..
DKT. ZAJA OMBOGA Tarehe

Sahihi………………………….............. ……………………………..
DKT.HANAH MWALIWA Tarehe

## TABARUKU

Tasnifu hii naitabarukia wazazi wangu Bw. Christopher Wanjala na marehemu mama Rose Apondi walionilea na kunionyesha milango ya darasa. Wangalinipuuza nisingalikuwa nilipo na nilivyo sasa. Tabaruku nyingine ni kwa mwanangu Shanice Rose na dadangu Judith Anyango kwa kunitunza na kuniunga mkono kwa hali na mali wakati wa kipindi kigumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu. Ninatakia heri na baraka za mwenyezi Mungu wale wote walio hai.

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia karama yake ya uhai, hekima na busara. Bila haya yote hatungeweza kufikia kiwango ambacho tumefikia kwa hivyo hatuna budi kumshukuru. Ningependa kuchukua fursa hii kutoa shukrani za dhati kwa wasimamizi wangu Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Hanah Mwaliwa kwa kujitolea kwao kuniongoza na kunipatia mwelekeo uliozalisha mafanikio ya kazi hii. Haingekuwa kazi rahisi kuandika tasnifu hii bila ushauri na uongozi wao.

Nawashukuru wahadhiri wangu wote walionifundisha tangu nijiunge na masomo ya uzamili mwaka wa 2012. Wahadhiri hawa ni Prof. Kineene, Prof. Habwe, Prof. Mbatiah, Dkt. Iribe, Dkt. Mweri, Dkt. Swaleh, Bw. Mungania, miongoni mwa wengine.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee ndugu zangu George, Gladys na Judith kwa kunitia moyo wakati nilipokuwa nikisoma. Bila kuwasahau rafiki na walimu wenzangu Mediatrix Ochieng na Walter Okuku. Shukrani nyingine ziwaendee wanafunzi wezangu tuliosafiri katika chombo kimoja na kuhakikisha kuwa tumefika mwisho wa safari licha ya vizingiti kadhaa njiani. Nao ni Gladys, Lydiah, Dinah, Sito na Marisya.

Shukrani nyingine maalum ziwafikie waumini wa kanisa la Christco-Funyula, chini ya uongozi wa Pastor Kepher Odinga kwa maombi yao yaliyonifikisha kumaliza safari hii ya uzamili. Mwisho ningependa kuwashukuru Charles na Evelyne kwa kuipiga taipu kazi hii na kuhakikisha kuwa imekamilika katika wakati unaofaa.

## IKISIRI

Utafiti wetu umeshughulikia usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule za Kiswahili ambazo ni *Asali Chungu* (S.A. Mohamed), *Anasa* (Y. King'ala) na *Fahari ya Mateso* (J.S. Oyoo). Uhusika wa vijana katika riwaya tatu teule unaelezea jinsi vijana wa jinsia zote walivyotelekezwa katika jamii. Wahusika vijana wametumika kama mbinu mahususi ya kuwasilisha jumbe za aina maalum ambazo zinaweza kuwa na athari kubwa katika jamii ya mwandishi. Kutokana na utafiti wetu, matatizo ya kijamii na kiuchumi huchangia pakubwa changamoto miongoni mwa vijana.

# YALIYOMO

**UKURASA**

**UNGAMO** ........................................................ **ii**

**TABARUKU** ........................................................ **iii**

**SHUKRANI** ........................................................ **iv**

**IKISIRI** ........................................................ **v**

**YALIYOMO** ........................................................ **vi**

**SURA YA KWANZA** ........................................................ **1**

1.0 Utangulizi ........................................................ 1

1.1 Tatizo la utafiti ........................................................ 4

1.2 Madhumuni ya utafiti ........................................................ 5

1.3 Maswali ya utafiti ........................................................ 5

1.4 Sababu ya kuchagua mada hii ........................................................ 6

1.5 upeo na mipaka ya utafiti ........................................................ 6

1.6 Msingi wa nadharia ........................................................ 7

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................................ 13

1.8 Mbinu za utafiti ........................................................ 15

1.8.1 Njia za ukusanyaji data ........................................................ 15

1.8.2 Uchanganuzi wa data ........................................................ 16

**SURA YA PILI: UHUSIKA NA WAHUSIKA VIJANA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI ........ 17**

2.0 Utangulizi ........ 17

2.1 Dhana ya uhusika ........ 17

2.2 Aina za wahusika ........ 24

2.2.1 Wahusika duara ........ 25

2.2.2 Wahusika bapa ........ 27

2.2.3 Wahusika vijana ........ 28

2.2.4 Wahusika shinda ........ 34

2.2.5 Wahusika wazazi ........ 34

2.2.6 Wahusika wa kihalisia ........ 35

2.3 Hitimisho ........ 36

**SURA YA TATU: MCHANGO WA ASASI ZA KIJAMII KATIKA MALEZI YA VIJANA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI ........ 37**

3.0 Utangulizi ........ 37

3.1 Asasi ya Elimu ........ 38

3.2 Asasi ya ndoa ........ 40

3.3 Malezi na afya miongoni mwa vijana (Asasi ya afya) ........ 49

3.4 Makazi yanavyoathiri vijana ........ 51

3.5 Ukosefu wa ajira ........ 55

3.6 Mahitimisho ........ 57

**SURA YA NNE: MAUDHUI NA UTAMBULISHO WA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA ASALI CHUNGU, FAHARI YA MATESO NA ANASA ................. 58**

4.0 Utangulizi ..................................................................................................... 58

4.1 Wahusika katika ujenzi wa maudhui na utambulisho wa vijana ............................... 58

4.1.1 Dhuluma na Unyanyaswaji wa vijana ..................................................................... 59

4.1.2 Madhara ya ulevi ..................................................................................................... 60

4.1.3 Ujasiri kama wasifu wa vijana .................................................................................. 60

4.1.4 Elimu ..................................................................................................................... 61

4.2 Mbinu za lugha na utambulisho wa vijana ............................................................... 62

4.2.1 Majazi ..................................................................................................................... 63

4.2.2 Taswira ................................................................................................................... 64

4.2.3 Matumizi ya Tashbihi .............................................................................................. 65

4.2.4 Methali ................................................................................................................... 67

4.2.5 Maswali ya Balagha ................................................................................................ 69

4.2.6 Mandhari na ujenzi wa maudhui katika malezi na utambulisho wa vijana ........... 70

**SURA YA TANO:MUKHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........................................................................................................... 73**

5.0 Utangulizi ..................................................................................................... 73

5.1 Mukhtasari ............................................................................................................... 73

5.2 Matokeo ................................................................................................................... 74

5.3 Mapendekezo ........................................................................................................... 75

**MAREJELEO ............................................................................................................. 76**

## SURA YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wetu unahusu usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule ambazo ni *Asali Chungu* (1977), *Anasa* (1984) na *Fahari ya Mateso* (2013). Kwa mujibu wa Kennedy (2007 ) dhana ya ujana ni kipindi kati ya utoto na utu uzima, unaelezwa kama kipindi cha maendeleo ya kimwili na kisaikolojia kuanzia mwanzo wa kubalehe kwa ukomavu na mwanzoni mwa utu uzima. Ufafanuzi wa umri maalum wa ujana hutofautiana. Pia anaangazia sifa za ujana zifuatazo: hali ya nia ya kufanya jambo fulani, hali ya ujasiri juu ya upole, hali ya mapenzi, hamu katika maisha ya raha na ubora wa ubunifu.

Naliaka (2012) anaelezea dhana ujana kwa mujibu wa umoja wa kimataifa (2011) kuwa ni mabarubaru wa jinsia zote ambao umri wao ni baina ya miaka kumi na mitano hadi ishirini na nane; kwa hivyo kwa maoni yetu, dhana ujana ni muda kati ya maisha ya mtu kati ya utoto na utu uzima. Ufafanuzi wa umri maalum hutofautiana katika jamii moja hadi nyingine.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999) taswira ni mkusanyiko wa picha zinazotokana na ufundi wa msanii katika kuteua na kupanga maneno yake ya kazi fulani ya kifasihi. Vilevile, taswira ni mkusanyiko wa picha anazozipata msomaji au msikilizaji wa kazi fulani ya kifasihi. Picha hizi huwa na funzo au ujumbe fulani.Katika utafiti wetu tutachunguza usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule, kwa kuongozwa na malengo ya utafiti wetu. Tutachunguza suala la malezi na asasi mbalimbali za kijamii zinavyowasawiri vijana na jinsi wanavyojitambulisha katika jamii

ya mwandishi. Malezi ni mchakato changamano unaojumuisha mambo kadhaa yakiwa pamoja na lishe, mavazi, makao, elimu pamoja na ushauri ambao ni mwafaka. Dhana ya utambulisho ni pana mno kwa sababu inafumbata mambo mengi ndani yake. Utambulisho ni jumla ya vigezo maalum vinavyotumiwa kumtambulisha mtu, kundi la watu, jamii moja au taifa fulani. Vigezo hivi hubainisha kuwa kundi fulani ni tofauti na lingine, jamii moja ni tofauti na nyingine, mtu mmoja ni tofauti na mwingine au taifa moja kuwa tofauti na lingine, haya ni kwa mujibu wa Kihore na wenzake 2009. Vigezo hivi ambavyo vinabainisha utambulisho wa mtu au jamii vinaitwa vibainishi.

Tobouret-Keller (1989) anaelezea kuwa utambulisho wa mtu umefungamana na mambo mengine kama vile lugha, utamaduni, mavazi, vyakula, dini, historia ya jamii, siasa, uchumi na kadhalika. Tunachomaanisha hapo juu ni kuwa, kipengele kimoja au viwili havitoshi kubainisha utambulisho wa mtu, jamii au taifa.

Mashirika mawili ya Umoja wa Mataifa UNICEF na UNESCO (2002) yanasema kiasi cha vijana milioni 30 kusini mwa Sahara hawaendi shule kwa sababu ya umaskini na mizozo ya kivita inayokumba bara la Afrika. Takwimu hizo mpya zimetolewa katika ripoti zilizochapishwa na shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na elimu, sayansi na utamaduni (UNESCO). Mashirika haya yanazidi kusema kuwa mgogoro wa kiuchumi duniani na mizozo ya vita barani Afrika vinafifiza juhudi za kuwarejesha vijana hao shuleni. Katika maeneo yenye vita mazingira yamekuwa hatari zaidi kwa vijana kufika shule.

Tutajikita kwenye riwaya tatu teule na kuzitumia kama kielelezo hata ingawa tutarejelea matini zingine ambazo zina maudhui yanayokaribiana kwa sababu mambo ya kimsingi ya kibinadamu ni yale yale tu, ila mazingira ndiyo hutofautiana. Changamoto zinazowakabili vijana zinaweza kutofautiana kimaeneo lakini ukweli ni kwamba zipo ulimwenguni kote. Jamii tofauti zimeweka mikakati ya kutafuta matatizo yanayowakabili vijana lakini hata hivyo utamaduni ni kizingiti kikubwa katika suala hili, hasa ulimwengu wa tatu. Juhudi nyingi zimefanywa na wanaharakati wasomi ili kuwasawiri vijana wa jinsia yeyote ile kuwa sawa katika jamii, lakini juhudi hizo hazijafaulu kwa kiasi kikubwa. Kuna mambo ya ukale na usasa ambayo yameleta athari katika malezi ya vijana wa kike na kiume katika jamii, tutachunguza kama ni hasi au chanya kuegemea kigezo cha familia hasa kutoka kwa matini teule.

Majukumu ya vijana katika jamii yamekuwa yakibadilikabadilka jinsi hali ya kijamii inavyobadilika. Katika mfano wa kiasili vijana wa kiume waliandamana na wazazi wao wa kiume waliowafunza shughuli za kiume. Wasichana nao walifundishwa mambo ya unyago yaliozingatia utekelezaji wa majukumu yao.Wakati huo changamoto miongoni mwa vijana zilikuwa kwa ufinyu kwa sababu jamii iliwajibika, kwani kuwaelekeza vijana ilikuwa ni jukumu la jamii nzima. Majilio ya wageni na wakoloni kutoka nchi za magharibi ulivuruga mifumo ya ulezi ambayo ilikuwako na maadili katika jamii.

Vijana hukua katika hali tofauti pamoja na kuwa na matumaini na mielekeo tofauti. Hawapo tu kama kikundi kimoja maalum, kwa hivyo kuna haja kuelewa kinachotendeka maishani mwao. Katika enzi hii yenye mabadiliko ya kimaumbile na ya kisaikolojia

ambayo huwakumba vijana maishani kupitia fasihi ya Kiswahili na kuelewa namna ambayo mabadiliko hayo huibuliwa na asasi za kijamii na kutekelezwa na watu wazima ni muhimu pia.

## 1.1 TATIZO LA UTAFITI

Utafiti huu unahusu usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili. Uhusika wa vijana katika lugha ya Kiswahili una upekee wa aina maalum-unaelezea jinsi vijana wa jinsia zote walivyotelekezwa katika jamii, kama njia ya kutafakari maswala nyeti ya kijamii na kama njia ya kutafakari michakato ya mitagusano ya kijamii.Vilevile, utafiti huu unanuia kubaini ni sababu gani zilizochochea baadhi ya waandishi kutumia vijana. Ni muhimu pia kujaribu kuelewa kwa kuonyesha kama vijana wanatumiwa kama mbinu mahususi ya kuwasilisha jumbe za aina maalum inapozingatiwa kwamba jumbe zinazowasilishwa kwa mitazamo ya vijana zinaweza kuwa na athari kubwa katika maudhui, mada na mawanda mengine anuwai.Utafiti wenyewe utaangazia jinsi malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana katika jamii.

Mitagusano katika maisha na mazingira yenye utata huwafanya vijana wajitambue na hata kufanya maamuzi yasiyofaa. Hata hivyo, kupitia uhusika wao kuna ufunuo wa taswira, maana ya ujana na changamoto zinazowakumba. Uhusika wao unasawiri tajriba maishani, hisia ya vijana na watu wazima na namna uhusika huo unavyozua changamoto za ujana katika malezi yao.

Masuala ya watoto na vijana yameshughulikiwa kwa kiasi fulani katika riwaya ya Kiswahili yakiwemo elimu, ubaguzi, kukosekana kwa usawa, saikolojia na sosholojia miongoni mwa mengine. Maongezi kuhusu vijana na yanayozingira jinsia ya kike na kiume yamewavutia watafiti wengi wa fasihi wakiwemo Mutua (2007), Naliaka (2012), Wamalwa (2013) na  Wahakiki wengi wa fasihi walizingatia maswala ya jinsia wamechunguza swala hili pasi na kushughulikia jinsia za kiume na kike kwa pamoja kwa minajili ya kupata kuzilinganisha.

## 1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Tunadhamiria kuchambua riwaya tatu teule; *Asali Chungu* (S.A. Muhammed 1977), A*nasa* (King'ala, 1984), na *Fahari ya Mateso* (Oyoo, 2013) kwa kuangazia usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili ili: -

1. Kutathmini matatizo yanayowakumba vijana wa jinsia ya kike na kiume katika riwaya tatu teule za Kiswahili.
2. Kuonyesha mchango wa asasi za kijamii katika malezi ya vijana wa jinsia ya kike na kiume katika matini teule.
3. Kutathmini kama jamii katika riwaya tatu teule zinawachukulia vijana wa jinsia ya kiume na wa kike kwa usawa.

## 1.3 MASWALI YA UTAFITI

1. Je, ni matatizo yapi yanayowakumba vijana katika riwaya teule za Kiswahili?
2. Ni jinsi gani asasi mbalimbali za kijamii zimechangia katika malezi ya vijana wa jinsia ya kike na kiume katika matini teule?

3. Jamii ya mwandishi inawasawiri vijana wa jinsia ya kike na kiume kwa usawa?

## 1.4 SABABU YA KUCHAGUA MADA HII

Tumeshughulikia maswala ya vijana kwa sababu tumegundua kuwa miongoni mwa vijana kuna mambo mengi hasi yanayoshuhudiwa nao hasa yanayohusiana na maadili miongoni mwao na tungependa kujua chimbuko la hali hizi kwa mkabala wa malezi. Kwa mfano uhalifu, matumizi ya mihadarati, ulevi na hata uzinzi. Sababu nyingine ni kuwa kundi tunalolishughulika lina umuhimu mkubwa katika jamii ambalo ni vijana. Asilimia kubwa katika jamii inawakilishwa na wao kwani hali ya siku zijazo zikiwemo uongozi unawategemea. Hao ndio kizazi cha kesho na viongozi wa baadaye.

Sababu nyingine ya kufanya utafiti huu ni kubaini chanzo cha vijana kukosa maadili wakiwa na umri mdogo sana. Kwa mfano: vijana wa kike kupata mimba za mapema na vijana wengine kunywa pombe katika umri mdogo. Katika msingi wa maisha ya kitamaduni maadili yalisambazwa na kuhimizwa miongoni mwa vijana, basi iweje kuzorota kwa maadili jinsi hii? Tutajishughulisha na kutafitia ukosefu wa malezi bora kama unavyochangia katika changamoto zinazowakumba vijana katika jamii. Utafiti huu pia utawapa watafiti motisha ya kulinganisha na kulinganua maswala mbalimbali ya vijana wa zamani na kisasa ili kubainisha tofauti zilizopo.

## 1.5 UPEO NA MIPAKA YA UTAFITI

Katika utafiti huu tunajishughulisha na riwaya hizi tatu; *Asali Chungu* (Mohamed, 1977), *Anasa* (King'ala, 1984),) na *Fahari ya Mateso* (Oyoo, 2013). Utafiti wetu unahusu

usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule. Tutaongozwa na madhumuni ya mada hii katika kufanya utafiti wetu.Tutaangazia matatizo yanayowakumba vijana, jinsi malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana kupitia asasi mbalimbali za kijamii na kama mwandishi amewasawiri vijana wa jinsia ya kike na kiume kwa usawa. Tutatumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi katika utafiti wetu kwa sababu huangazia mamlaka na nguvu kama mihimili ya kijamii.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ina chimbuko lake nchini Urusi na kuasisiwa na George Lukacs (1916). Nadharia hii hutazama kazi yoyote ya sanaa kwa kuzingatia hali ya jamii inamozaliwa na kukuzwa sanaa hiyo. Tumeishugulikia kazi hii tukiongozwa na nadharia ya 'Sosholojia ya Fasihi' Lukacs alirithi mawazo ya maendeleo ya kijamii na migongano ya kitabaka kutoka kwa Karl Marx kwa mujibu wa Coser L. (1963) Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalumu cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina ya kazi ya sanaa, umma na muundo wa kijamii na jinsi kazi hiyo imejitokeza na kutathminiwa ubora na uhafifu wake. Hunuia kueleza sababu ambazo zimechangia kuibuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo la kijamii na jinsi fikra za ubunifu wa mwandishi huongozwa na mila, desturi na mpangilio wa jamii husika (Hii ni tafsiri yetu).

Kulingana na Coser (1963), binadamu ndiye kiumbe pekee aliye na uwezo wa kutumia lugha. Kwa miaka mingi iliyopita, binadamu amekuwa akijishughulisha na ukusanyaji wa maarifa pamoja na kanuni za mwenendo maishani. Haya yote yameweza kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Anatamatisha kauli hii kwa kusema kwamba ni jamii

za kibinadamu pekee zilizo na uwezo wa kuwa na mila. Tylor E kama alivyonukuliwa na Coser (1963). Kuhusu Sosholojia ya Fasihi alitoa mchango kuhusu dhana ya utamaduni kwamba, ni dhana isiyoweza kuelezwa kwa urahisi kwa sababu ni changamano. Inahusu imani, mila, desturi, itikadi, maadili, sheria, elimu pamoja na mazoea ambayo mtu huwa nayo kama mmoja wa wanajamii. Vipengele hivi ni muhimu kwetu kwa sababu vitatusaidia kuangazia malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya teule.

Jamii zote zinajulikana zimeweka wanajamii katika matabaka kihadhi. Kuna tabaka la juu, kati na chini. Mchakato huu unahusu ugavi wa majukumu ya kila mtu kiumri, kijinsia na kihadhi huku tofauti ikibainika wazi kupitia umiliki wa mali, mamlaka na ukuu. Tofauti kati ya tabaka la juu na la chini, matajiri na maskini, watawala na watawaliwa, wenye nguvu na wanyonge ni vigezo vinavyotumiwa kuainisha makundi haya. Jinsi wanajamii katika makundi haya wanavyochukulia na kuhudumiwa, wanavyogawiwa majukumu na ukosefu wa haki sawa hubainisha mfumo wa kijamii.

Sosholojia ya Fasihi pia huangazia mamlaka na nguvu kama mihimili ya kijamii. Kwa mujibu wa Coser (1963), mamlaka ni uwezo wa kuamua mwenendo au tabia ya watu wengine kulingana na matarajio ya mwenye mamlaka. Hakuna mahusiano ya kijamii ambapo elementi ya mamlaka itakosekana kabisa, hivyo basi kuna fikra kwamba dhana ya mamlaka ni msingi katika dhana zote za kisosholojia kwa kifupi, mamlaka ni zile nguvu ambazo mtu hupewa kulinga na kaida zinazokubalika na watu wawili au zaidi na kati ya makundi mawili au zaidi kwenye mahusiano. Coser (1963) anamnukuu Max

Weber aliyeainisha mamlaka na kuyaweka katika makundi matatu ambayo ni mamlaka ya kisheria, mamlaka ya mila na desturi (mapokeo) na mamlaka ya kihaiba (charismatic).

Narizvi (1982) aliandika kuwa uhusiano baina ya fasihi na jamii umekuwa mada ya mvuto katika uchunguzi wote wa kibinadamu. Wahakiki wa kazi zilizoandikwa na wanasosholojia wamekuwa wakijadili mada hii kutokana na mitazamo mbalimbali na kutoa kauli mbalimbali zenye ukweli kinzani kiasi cha kukanganya mtu aliye na tajiriba katika nyanja mahususi.

Kulingana Wellek na Warren (1954), uhusiano baina ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kutanguliza ufungamano wa fasihi na jamii. Wahakiki wa dhana hii wanadai kuwa ni makosa kuchukua fasihi kama kigezo cha kuashiria jinsi jamii yeyote ile ilivyo. Walidai kuwa kazi kama zile za mwandishi maarufu Shakespeare na tenzi za Milton au kazi ya Burke haziwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha jamii zao. Jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea tajiriba, uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha hivyo basi itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka. Mtazamo wa fasihi kupitia sosholojia, hutufanya tumchukuwe mwandishi kama zao la nguvu za kisosholojia za wakati wake na kuepuka kumpunguzia sifa za ubunifu asilia. Kulingana na James Sutherland (1957), jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopokea pamoja na dini yake.

Upingamizi mwingine kuhusu matumizi ya elimujamii ya fasihi ni mtazamo wa mwandishi na nguvu za kisosholojia ambazo huchunguza sehemu teule na hivyo kuufanya mtazamo wa kijumla kukosa maana. Wahakiki walishikilia dhana kwamba uchunguzi wa fasihi unahitaji tuwe na wazo kuhusu kile ambacho ni muhimu na kile ambacho si muhimu. Wahakiki wanaopinga mbinu ya kisosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi upande mmoja na hali ya kijamii, uchumi na siasa upande mwingine.

Uchunguzi wa kijamii kuhusu kazi ya maandishi au mwandishi mwenyewe utatusaidia kumchunguza mwandishi kama mwanachama wa jamii, athari za kijamii zilizomwathiri na kumpatia msukumo wa kubuni kazi ya sanaa. Kwa mfano, sisi tutachunguza kazi za Oyoo (2013) King'ala (1984) na Muhamed (1977) ambazo ni za kisanaa. Sosholojia ya Fasihi inamzingatia binadamu kama uti wa mgongo wa ulimwengu huu na sanaa kwa ujumla wake. Ndio maana tumeichagua nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kutupatia msingi kuzichambua na kuzichanganua riwaya za *Anasa*, *Fahari ya Mateso* na *Asali Chungu*, kwa kuegemea mihimili yake.

Kazi za Wellek na Warren (1978) zinabainisha uwezo wa Sosholojia ya Fasihi kwa kuchanganua maswala ya malezi ya vijana katika matini teule. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi itatufaa kwa kazi hii tunayoishughulikia. Kwa mujibu wa Wallek na Warren (1978),

> Fasihi imeibuka kutokana na uhusiano wa karibu na taasisi za kijamii na jamii duni. Ni vigumu kutofautisha ushairi na ibada, mazingaumbwe na kazi au igizo. Fasihi pia ina dhima katika jamii na haiwezi kuwa ya mtu binafsi, hivyo basi, maswala mengi ambayo huibuka kupitia uchunguzi wa kifasihi huwa ya kijamii. Kwa mfano maswala kuhusu mila, kaida, hadithi, msimbo na visasili.(tafsiri yetu)

Kama nadharia yoyote ile, Sosholojia ya Fasihi ina wale wanayoipinga. Wapizani wake wanadai kwamba nadharia hii haitatusaidia kuchunguza uhusiano baina ya fasihi na mambo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa kwa sababu uhusiano hauwezi kujitokeza wazi katika kitengo chochote kile hata hivyo basi umuhimu wake hauwezi kutathminiwa.

Maelezo ambayo tumetoa kumhusu Georg Lukacs yanatokana na athari ya itikadi za Ki-Marx. Mawazo ya wanafalsafa kama vile Pierre Macherey, Terry Eagleton na Fredrik Jameson pia yalitoka kwa *Marx* na ya kuelekezwa kwa fasihi ya wakati huo. Mawazo ya Lukacs ya kuchapisha maandishi kuhusu nadharia ya Sosholojia ya Fasihi (1916) yalitetea mwamko uliosababisha kuanzishwa kwa shule ya Frankfurt mnamo mwaka wa (1923) na wanasosholojia wa vitengo vyote vinvyohusiana na Sosholojia.

Sosholojia ya Fasihi huchukulia kuwa maisha ni vitendo, ni ubunifu unaodhamiria kuendeleza uwezo alionao binadamu wa kushindana na mazingira. Nadharia hii huzungumzia raha kuu ya kuishi ulimwenguni ambayo lazima binadamu afanye awezalo kuilinda ili kuweza kuishi kama muungano wa jamii moja ya kibinadamu.Vijana wanapokuwa hujihusisha au kujitambulisha na kikundi fulani ambacho huwazia kuwa kina tabia inayomvutia. Ikiwa ni walioacha shule hutembea pamoja, wahalifu pia. Kwa hivyo sosholojia ya fasihi hujishughulisha na matukio ya wakati ujao yaani yaelezea uundaji wa jamii mpya yenye furaha na iliyojengeka kwenye misingi ya kisosholojia.

Mara nyingi tunawaona vijana wakipuuza tamaduni za kiasili na kuchukua mwelekeo wa kisasa katika jamii. Mara nyingi tunawaona wakijifanyia uamuzi bila kutafuta ushauri kutoka kwa wazazi wao.

Ukweli kuhusu maisha ya binadamu lazima ufahamike kwake na wenzake wote ili kwa pamoja waweze kuleta mabadiliko kwa manufaa ya jamii nzima. Jukumu hili ndilo linalosisitizwa na Sosholojia ya Fasihi. Ni vyema vijana wahusishe washikadau katika mipango yoyote wanayowazia kuifanya ili kukuza jamii yenye muungano uliosawa.

Nadharia hii pia huangazia kama mwandishi asilia ana matumaini kuhusu hali ya siku zijazo za jamii yake katika kujiendeleza na kujiondoa kutokana na hali fulani. Kuhusu swala hili Lukacs (1962) anasema:

> Sanaa ya kijamii haitosheki na mtazamo ulio hafifu…..
> jukumu lake ni kuonyesha kuzaliwa kwa kesho na kutokana
> na leo na matatizo yanayoandama na kuzaliwa huku(tafsiri yetu)

Vijana ndio viongozi wa kesho kwa hivyo jamii inastahili kuwaelekeza katika njia inayostahili. Lukacs anatupa mawazo mengi yanayofaa mwafaka uliopo kati ya sanaa na jamii kutoka enzi za kale hadi leo. Dhana ya Sosholojia ya Fasihi inamtarajia msanii auwasilishe uhalisi wa maisha katika hali yake ya maendeleo na kimapinduzi kikweli na kuzingatia historia . Mikinzano yoyote ya kijamii huchangia katika kuyaleta mabadiliko hayo.

Tukirejelea madhumuni ya tasnifu yetu nadharia hii itatufaa zaidi kutathmini matatizo yanayowakumba vijana katika jamii ya mwandishi. Nadharia hii itatusaidia kuangazia changamoto za vijana katika jamii na hujitokeza katika uteteaji wa wanyanyaswaji.

Antonio Gramsci (1927) alitilia mkazo katika kuonyesha maendeleo ya nadharia hii kwa mtazamo wa umakisi wa kisasa kando na mtazamo wa awali wa kiuchumi. Alisisitizia mapinduzi dhidi ya ubepari kwani watu walihitaji sana usaidizi kutoka kwa wanajamii wasomi.

Wapingamizi wa nadharia hii hawakuridhika na suala la nadharia hii kuangazia maswala ya kiuchumi pekee kwa kuangazia hali ya jamii. Walisema kuwa nadharia hii ingeangazia pia maisha katika jamii. Wanasosholojia wa kikundi cha Frankfurt,anavyoelezea Zoltan (1973) waliangazia jamii kwa ujumla na sio maswala ya mtu binafsi.

## 1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA

Muindi (1990) alitafitia ukahaba katika riwaya za Said Ahmed Mohamed. Jambo ambalo lilijitokeza ni kuwa Muindi alirejelea tu madhara kwa vijana wa kike .Tofauti na utafiti wetu, ulizingatia athari ya ukahaba kwa vijana wa kike na kiume. Pia suala la ukahaba ni baadhi ya changamoto zinazozuia juhudi za vijana kutojiendeleza. Kwa hivyo kipengele cha ukahaba kitatufaa katika utafiti wetu wa usawiri wa jinsi malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana.

Katola (2006) alishughulikia suala la udhalimu dhidi ya wahusika wa kike kama unavyojikita katika kazi za waandishi wa jinsia zote mbili katika tamthilia za Kiswahili. Ingawa amelenga tu wahusika wa kike, sisi katika utafiti wetu tunaangazia dhuluma ambazo vijana wanatendewa katika jamii bila kuegemea jinsia moja. Basi pengo hilo la

kutoangaziwa kwa matatizo yanayowakabili vijana kwa ujumla bila upendeleo au kuutilia uzito jinsia moja ndilo lile ambalo utafiti wetu unanuia kuziba.

Nkonge (2006) ameshughulikia athari za udhanaishi katika riwaya ya Kichwa Maji (1974) na Nguvu ya Sala (Wamitila 1999). Baadhi ya mambo ambayo ameshughulikia kuhusu vijana ni kama mapenzi na ndoa, maisha na kifo, malezi, uozo wa jamii na dini. Masuala haya yanaoana na baadhi ya yale ambayo tunayashughulikia katika utafiti huu kwa hivyo kazi yake imekuwa ni ya manufaa makubwa kwetu. Tofauti ni kwamba huku akitumia nadharia ya udhanaishi sisi tumetumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

Mtua (2007) ameangazia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi wa mwanamke katika tamthilia tatu za Kiswahili. Kilichotuelekeza kupitia kazi hiyo ni mitazamo ya vijana katika ukombozi wa wanawake pekee. Katika utafiti wetu kuhusu usawiri wa jinsi malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana katika rawaya ya Kiswahili, tulihisi kwamba ukombozi ambao vijana wanahitaji uwe ni wa malezi, ajira au elimu unafaa kushughulikia vijana wote bila kujali jinsia zao .

Naliaka (2012) alitafitia uhakiki wa hali ya vijana katika riwaya ya vipanya vya Maabara akitumia Nadharia ya uhalisia. Alizungumzia matatizo yanayowakumba vijana. Baadhi ya vipengele alivyovizungumzia ni mapenzi, dawa za kulevya, ukosefu wa ajira, ubakaji, uhalifu kama maswala nyeti katika jamii. Masuala aliyoyataja yatatusaidia katika kushughulikia maswali ya utafiti wetu ambayo yanazungumzia changamoto zinazowatatiza vijana katika jamii. Utafiti wake unafanana na wetu kwa kuwa

unashughulikia vijana wa jinsia zote, tofauti iliyopo ni kuwa alitumia nadharia ya uhalisia nasi tuliongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi pamoja na matumizi tofauti ya riwaya.

Wamalwa (2013) ameshughulikia uchanganuzi wa changamoto za ujana katika riwaya za Habwe. Alitumia nadharia ya Uhistoria Mpya katika utafiti wake. Changamoto alizozitaja kama vile, ulevi, umaskini, usherati na uvivu zitatusaidia katika utafiti wetu unaojishughulisha na jinsi malezi yanavyoathiri utambulisho wa vijana. Tofauti iliyoko ni kuwa katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

## 1.8 MBINU ZA UTAFITI

### 1.8.1 Njia za ukusanyaji data

Utafiti wetu ulifanyiwa maktabani. Tulisoma na kuchanganua riwaya tatu teule ambazo ni *Asali chungu* (1977), *Anasa (*1984) na *Fahari ya Mateso* (2013) ili kupata maelezo kuhusu usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika jamii ya waandishi husika. Uchunguzi wa kina ulifanywa kuhusu nadharia ya Sosholojia ya Fasihi katika vitabu, tasnifu, majarida kwani ndiyo itakayo tuongoza katika utafiti wetu. Njia nyingine ya ukusanyaji data ni kutalii mtandao ili kusoma masuala muhimu yanayohusiana na malezi ya vijana pamoja na changamoto zinazowakumba. Tutashauriana na wataalam mbalimbali ambao pia ni wakufunzi wa fasihi katika idara chuoni ili kupata ushauri zaidi kuhusu mada yetu ya utafiti

### 1.8.2 Uchanganuzi wa data

Baada ya kusoma na kuchanganua matini tatu teule na kuangazia changamoto wanazopitia vijana, tumechanganua masuala kwa misingi ya madhumuni ya utafiti. Utafiti stahilifu umetufaa kwa kazi hii kwa sababu malengo yetu yanashughulikia matatizo yanayowakumba vijana kama ukosefu wa ajira, umaskini, ulevi na ukosefu wa maadili tukirejelea riwaya teule, kuonyesha mchango wa asasi ya kijamii katika malezi ya vijana na kuonyesha kama jamii inawasawiri vijana wa kike na kiume kwa usawa.

# SURA YA PILI

# UHUSIKA NA WAHUSIKA VIJANA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii inazungumzia uhusika wa vijana katika riwaya ya Kiswahili. Tunashughulikia suala hili tukijitika katika matini tatu teule ambazo ni *Fahari ya Mateso* (Oyoo .S 2013), *Anasa* (Kingala Y.M. 1984) na *Asali Chungu* (Said A.M. 1977). Wakati mwingine waandishi huwasawiri wahusika namna wafanyavyo ili kutafuta uhalisi wa kifasihi kwa vile fasihi ina ubunifu mwingine ambao wakati mwingine hutueleza kuyachukulia kama mambo ya kidhahania yasiyoweza kutwekwa katika njia ya kawaida kwa vile vijana ndio wahusika ambao wamechukua sehemu kubwa ya riwaya hizi. Ilitubidi tuangazie kwanza suala pana la uhusika na wahusika ili uwe ndio msingi wetu wa kusawiri jinsi malezi yanayovyoathiri utambulisho wa vijana katika matini tatu teule. Pia tutashugulikia mbinu ambazo watunzi walitumia katika kuwaumba na kuwainisha wahusika wao tukirejelea matini tatu teule.

## 2.1 Dhana ya Uhusika

Mbatiah (2001) anaeleza uhusika kama utaratibu na kuwaumba wahusika pamoja na kunga zinazokwenda na utaratibu huo hasa utofautishaji na ukuzaji wao. Uumbaji ni dhana inayoambatana na ubunifu mkubwa. Mbatiah anaendelea kusema kuwa uumbaji wa wahusika hutilia maanani dhamira ya mwaandishi. Tunaafikiana na maoni ya Mbatiah kwani msaani husisitiza kile kilichopo katika jamii yake na kile anachotaka kuonyesha kumfanya msomaji ajue kuwepo kwa haki, ukweli na maisha bora. Kwa kutegemea

mazingira na hali za kihistoria na kiutamaduni na kwa kutegemea ufahamu wa msanii kuhusu hali za maisha na aina za ufafanuzi wa maisha hayo.

Mhusika huumbwa kupitia kwa matendo yake katika kazi ya fasihi. Matendo haya ni kupitia kwa vitendo anavyofanya (tabia) au mazungumzo yake. Tunaongezea kuwa mhusika pia huumbwa kwa maelezo kumhusu. Mfano katika riwaya ya *Fahari ya Mateso,* Mateso alizubaishwa na urembo wa mmoja wa wahudumu wale. Msichana mwenyewe alikuwa na rangi ya maji ya kunde, nywele ndefu za singa, meno meupe pepepe yaliyo jipanga mithili ya lulu katika chaza. Aidha alikuwa na uso mwororo uliorembeshwa zaidi kwa macho ya kikombe yaliyodhibitiwa vyema na kope nyeusi tititi. Kwa juu nyeusi laini za upinde zilizoboresha wangavu wa uso wake hususan alipoonesha tabasamu iliyoashiria huruma aliangalia kifua cha binti huyo kilichotutumishwa na madodo, mikono ya mbinu na mwendo wa bata mzinga aeleaye kama ukufi bwawani vilifaulisha urembo wake (uk.62). Tutasema kuwa maelezo haya yanaashiria jinsi dada huyo alivyokuwa mrembo.

Kwa mujibu wa Mbatiah (2001) anasema kuwa uumbaji wa wahusika hutilia maanani dhamira ya mwandishi. Dhamira yake ni kumuumba kila mhusika kama kikale cha tabaka maalum. Kwa mfano katika *Anasa* mhusika Anasa ni kikale cha tabaka la makabwela, Ziporah ni kikale cha tabaka la mabwenyenye. Kila mhusika amesawiriwa kwa namna ambavyo anabainisha waziwazi sifa za tabaka lake. Katika uumbaji wa wahusika katika *Asali chungu,* Kamunde (1983) akishughulikia kilio cha wanyonge katika riwaya za S.A.Mohamed anasema kuwa amewachora wahusika katika matabaka.

Tabaka la mabwenyenye na tabaka la mafukara. Zuberi ndiye anayewakilisha tabaka la mabwenyenye hali wahusika wengine duni kama vile Dude, Semeni n.k wanawakilisha tabaka la makabwela.

Katika riwaya tatu teule, waandishi wamewasawiri wahusika kwa njia tofauti tofauti kwa lengo la kufanikisha maudhui yao . Amewaumba vijana wa kike na kiume ambao amewapa majukumu tofauti tofauti kulingana na nyadhifa walizopewa riwayani. Riwaya yoyote hutawaliwa na wahusika kufuatana na maono ya msanii ambaye hutawaliwa na uhalisi wa kifasihi kwamba anayoandika msanii yanaweza kuaminika. Katika matendo ya mhusika, msanii anaweza kusisitiza kile kilichopo katika jamii yake na kile anachotaka kuonyesha, kumfanya msomaji ajue kuwepo kwa haki, ukweli na maisha bora. Hivyo kwa kutegemea mazingira na hali za kihistoria na kiutamaduni, na kwa kutegemea ufahamu wa msanii kuhusu hali za maisha na aina za ufafanuzi wa maisha hayo, tunaweza kuona katika riwaya za wakati mmoja matendo tofauti ya wahusika. Matendo ya wahusika ndiyo msingi wa maudhui kwa hivyo lazima yaelezwe kikamilifu, kama kwamba wahusika hao ni watu halisi na matendo yao yanatuathiri moja kwa moja.

Wamitila (2003) anaiita mbinu ya kimuhtasari, ambapo mwandishi anaweza kutoa wasifu wa mhusika kiumbo au matendo. Hufanya hivi kimaelezo yeye mwenywe kama mwandishi au kutumia mhusika fulani kotoa wasifu kuhusu mhusika mwenzake. Wahusika vile vile wanaweza kuumbwa kwa matumizi ya kimajazi au majina ambayo yanashabihiana na sifa za huyo mhusika fulani inavyoelezwa na Wamitila. Tunalotaka

kusema ni kwamba  unawajibika kuhakikisha kwamba unamhusisha mhusika huyo ili atende vitendo au aseme mambo ambayo yanayoonyesha au kuangamiza jina ulilompa.

Kwa mfano, katika *Asali Chungu*

> "Hapa Baya huwa mke na Dude huwa mume. Na siku nyingine na nyingine  tena, huowana na kuowa na bila ya kikomo. Tena Baya humfundisha Dude yale aliyoyaona kwa mamake  na mtaa wake wapo kitandani pao (uk 37).

Kutokana na dondoo hili, jina Baya, ingawa linamtambulisha mhusika fulani, pia linatoa maelezo murwa kuhusu matendo ya mhusika huyo ambayo ni mabaya kama jina lake. Matendo haya ameyarithi kutoka kwa mama yake. Mhusika Baya, anaeleza maudhui ya ubaya katika mapenzi na uasherati.

Matumizi ya utendaji au ya kidrama pia hutumika kuwaumba wahusika. Katika matumizi ya mbinu hii mhusika huzungumza huku anatenda vitendo vile katika mawasaliano yake hutupa wasifu wake. Katika riwaya ya *Anasa*, tineja mmoja alirundikwa najisi na kuku aliyekuwa amepakatwa na mwanamke kikongwe. Aliposhuka katika hali ya kuinyosha suti yake, alikabiliana na najisi hii. Hasira zilimpanda na kumgeukia nyanya aliyekuwa amepakata kuku karibu naye.

> " Huna macho? Tineja alimfokea bikizee akiwa amemtolea macho makali." Pole mwanangu" Bi kizee alijibu. Sikiza, mimi si mwanao, akiyasema hayo alimjia nyanya huyu jongwajongwa na kuanza kumdunga pua kwa kidole cha shahada (uk. 76)

Tendo hili la tineja kumfokea nyanya linamsawiri kama mtovu wa maadili. Masuala kama haya yanajitokeza sana katika jamii na husababishwa na ulegevu wa wazazi kuwashauri watoto au vijana wao katika njia ambayo inafaa. Matumizi ya dawa za kulevya na vijana hasa wale ambao wameacha shule na kujiunga na vikundi ambavyo

vinajihusisha na uhalifu katika jamii. Vijana hujiingiza kwenye ulevi, wizi, uasherati na kadhalika. Wazazi pamoja na washikadau wengine katika jamii ikiwemo dini wanastahili kuchukua hatua ya haraka kuwapa vijana mwelekeo unaofaa kuhusiana na maadili na uhusiano wao katika jamii. Katika maisha ya kiasili, vijana walikuwa na maadili mema kwa sababu jamii ilikuwa na jukumu la kutimiza miongoni mwa vijana. Tunaona kuwa utamaduni hubadilika jinsi nyakati zinavyoathiriwa na mabadiliko ya kiteknolojia na utandawazi.

Mazingira wanamoishi vijana wa kike na kiume huwadhuru, pia huwafanya waonekane raia wabaya. Wazo linalojitokeza ni kuwa kila kitendo kina chanzo na lililopo basi ni kuwa badala ya vijana kupuuzwa, ni vyema suluhisho litafutwe kupitia chanzo cha majanga yanayowakumba. Maelezo haya yanaweza kusikika katika jamii. Hivyo inadhihirika kuwa fasihi kupitia riwaya huvuka mipaka ya wakati na mahali ili kutoa kauli zinazohusu matendo, tabia na maisha ya wanadamu.

Katika harakati za kuikataa mikatale ya unyanyasaji na unyonyaji wa vijana, mhusika huonyesha uhalisi zaidi kama amepewa nafasi ya kubadilika. Mabadiliko haya yanadhihirishwa na wahusika wengine kuhusu vijana.Wanafasihi huelezea matatizo na mafanikio ya jamii kama wanavyoyaona kulingana na tajriba zaidi. Mwandishi huyafichua matatizo ya jamii kwa kuyaweka katika lugha iliyowazi yenye kueleweka.
Wasanii huiangalia dunia wanayoishi na watu wa jamii zao. Hapo ndipo wanapozaliwa mawazo kutokana na hali halisi, waionayo wasanii. Msanii hutumia lugha kuweza kutoa fikra, rai, au falsafa zake akizingatia wahusika ambao huwekwa katika mazingira

yanayostahili kwa msomaji, hisi tofauti na mafundisho muhimu ili pale anapostahili aweze kukosoa.

Lugha ni kipengele muhimu kinachojenga kazi ya fasihi yoyote ile. Lugha ni wenzo wa fasihi, ni rasilimali ambayo huzalisha sanaa ya fasihi (Onchangu, 2013). Umuhimu wa lugha katika fasihi hupatikana katika maana iliyoeleweka na msomaji. Hivyo basi lugha ni msingi, nguzo na mihimili na kazi ya fasihi. Hapawezi kuwepo fasihi bila lugha. Mwandishi wa fasihi hutumia lugha ili kujieleza. Huwapa wahusika maneno ambayo wao huyasema kwa niaba yake na mwandishi huwa na maana ambayo inawasaidia kueleza yale ambayo yamekusudiwa na msanii. Lugha anayotumia mhusika huambatanishwa na picha zilizojengwa za mawazo ili kuweza kuleta athari kwa msomaji. Katika *Fahari ya Mateso,* Mateso, uk. 25 anajiuliza ilikuwaje hadi akajipata akitembea katika barabara za jiji la Nairobi. Kwa maoni yetu, lazima waandishi wa riwaya watumie lugha ili kuwasilisha ujumbe wao katika jamii lengwa.Yaweza kuwa lugha andishi au simulizi ambayo inaeleweka na walengwa. Kwa hivyo lazima mwandishi aelewe kiwango cha elimu cha kikundi anachokizungumzia.

Kufafanua umbo ni njia ya kumtambulisha mhusika. Katika riwaya ya *Anasa* (1984) mwandishi anaelezea umbo la mhusika Hawa hivi:

> “Kichueni, Mungu alikuwa kamtunukia shungi la nywele za singa, paji la uso wake alilojua kuling’arisha vilivyo lilibandikwa maji ya kikombe … Jamala ya sura yake ilikuwa ya kuwatia watu mboni … (Uk 5.)

Kupitia maelezo haya, picha ya vijana inawekwa wazi. Usawiri wa vijana katika utafiti huu unadhihirisha namna ambayo uhusika hubainishwa na mielekeo ya jamii. Ni kupitia uchoraji wa picha katika maelezo ambapo vijana wa kike na kiume hukua na kuwa kama mwanamke au mwanamume mkomavu mtawalia. Jamii husika ndiyo hutambulisha vijana jinsi anavyotaka kupitia kwa mwandishi. Maelezo haya ambayo mwandishi anayotoa ni miongoni mwa sifa za vijana katika ukuaji wao. Kwa hivyo walengwa huvutiwa na jinsi mhusika wa kundi  lao alivyoelezwa.

Wamitila vilevile, anaelezea kuwa wahusika wanaweza kuubwa kwa kutumia mbinu ya kisaikolojia ambayo inahusishwa na mazungumzo nafsia. Mara nyingi, mtu akiwa hali ya kutafakari au kukumbwa na matatizo mengi, huweza kuwaza kwa sauti kwa kujisemeza mwenyewe na tukapata hulka yake. Katika *Fahari ya Mateso*, Mateso anajijutia mbona akatelekezwa na kuhangaika maishani.

> "Jambo gani nililowakosea wazazi wangu hadi wakanitelekeza jinsi hii? Mama yangu ni nani na anaishi wapi? Mbona hawezi kukumbuka ……. Nikosa gani nilitenda hadi nikaachwa katika msitu huu uliojaa simba, fisi, chui….          (uk. 25)

Mateso anaendeleza maudhui ya mateso, anayajutia maisha anayoyapitia yaliyojaa changamoto nyingi kama vile ukosefu wa elimu, kurandaranda mitaani, wizi pamoja na ukosefu wa chakula ambao unadhoofisha afya yake. Vijana mara nyingi wanapojipata katika hali kama hizi huamua kutafuta njia zingine mbaya za kujitafutia lishe.  Mara nyingi huanza kuwanyang'anya watu pesa, simu na vibeti vya akina mama ili kupata kitakacho wafaidi. Kwa bahati mbaya wanaponaswa hupigwa na hata kufa au kushikwa na polisi na kufungwa.

Katika sehemu hii, imetupasa kuelewa dhana uhusika na jinsi msanii anavyoweza kuwaumba wahusika wake. Uhusika ndicho kipengee muhimu katika kazi yeyote ile ya fasihi kwa maana maudhui na dhamira itakikanavyo hutegemea aina ya wahusika ambao msanii amewabuni. Katika utafiti wetu tumeshugulikia usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana tukijikita katika matini tatu teule; itakuwa vyema tukishugulikia uainishaji na wahusika, kwani wao ndio hufaulisha kazi yeyote ya sanaa. Tutawatambulisha wahusika vijana kupitia kwa nafasi zao walivyoumbwa na msanii ili tupate kujua anapatikana katika kundi lipi kwa kutegemea vigezo au mikabala fulani.

## 2.2 Aina za Wahusika

Wamitila (2008) ametubainishia wahusika kuwa watendaji wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi ya kifasihi. Tutaainisha wahusika wetu kwa kuzingatia uthabiti na misimamo yao katika mwingiliano wao na wahusika wengine ambao wana mtagusano nao katika mazingira hayo. Vile tulivyosema hapo awali kuwa hakuna kundi fulani linaloweza kudai kujitosheleza na kujisimamia kuwa ni bora kuliko lingine. Anasema kuwa wahusika wamegawika katika makundi mawili makuu, kulingana na nafasi au majukumu anayowapa mwandishi. Wahusika wakuu hupatikana kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Wahusika hawa huwa wenye ukadiri mpana na wenye uchangamano wa sifa na aghalabu hukua kadri riwaya inavyokua. Katika *Anasa*, mhusika Hawa anaonekana mtoto mwenye maadili mema mwanzoni mwa riwaya. Kulingana na hali ya maisha anayopitia anaishia katika maisha ya anasa. Kwa hivyo mwandishi wa *Anasa* anawachora wahusika wake katika hali ya kukua. Hali hii inaifanya kazi ya fasihi husika kupata uyakinifu unaokamilika.

### 2.2.1 Wahusika Duara

Wahusika hawa huwa na sifa zinazokaribiana zaidi na binadamu wa kawaida katika jamii. Wanaweza kubadilika kutegemea hali ya maisha au mazingira ambamo wanaishi, hubadilika kitabia na pia kimawazo. Uduara unaweza kuwahusu wahusika wakuu na hata wasaidizi. Wahusika wakuu huwa na sifa changamano zinazokaribiana sana na za binadamu (waweza kutumiwa kueleza uovu au wema. Kwa mfano, Dude katika riwaya ya Asali *Chungu*, anaonyesha sifa za uduara. Tunamuona Dude tangu utotoni na tunamfuata riwayani hadi anapofikia utu uzima.

Tunaona mazingira ya kijamii yakikosa usawa kwake Dude kwani anabadilikabadilka. Maisha haya yanaweza kumdunisha mwanadamu na kuangamiza utu wake. Mfano: Dude na Baya wanaingilia mambo ya uzinzi tangu wakiwa wadogo, kwa sababu wazazi wao ni makahaba na wanayaona yote wanayoyafanya. Wanawaiga wazazi wao na hata wanapokuwa watu wazima, matendo ni hayo hayo. Tunamuona Dude tena ana huruma na wema wa roho. Dude alimchukua Baya aliyekuwa amelowa damu na kumpeleka hospitalini hata baada ya kukatazwa na 'bosi' wake Bi. Amina. Hiki ni Kitendo cha kijasiri kinachotokana na imani ya roho yake. Dude ni mhusika mviringo au duara. Tunaweza kusema kuwa katika jamii wahusika duara hujimudu katika hali au nyakati zozote za maisha.

Wahusika wakuu huchukua nafasi muhimu katika uendelezaji wa riwaya na hivyo maudhui makuu huwazunguka wao; Ni wahusika ambao hujitokeza mara kadhaa na hivyo kuwa na upana wanapolinganishwa na wahusika wajenzi (Rimmon na Kenan

2002) kufuatana na wazo hili katika *Fahari ya Mateso*, Mateso anaendeleza maudhui ya umaskini, bidii, wizi n.k. Mhusika huyu anajitokeza riwayani kwa upana akiendelea kukuzwa na wahusika wadogo.Wahusika wadogo wanakuzwa kwa ufinyu kwa mfano mamake Mateso (Bi. Riziki). Kupitia kwa wahusika wakuu mwandishi anaonekana akielezea yale ambayo anawania kusisitiziwa au kuepukwa katika jamii.

Mbatiah (2001) anachangia zaidi katika madai ya kumkuza mhusika. Anasema kuwa swala hili ni muhimu sana katika utanzu wa riwaya uliojikita katika uyakinifu. Anazidi kusema kuwa suala la kukua ni la kimaumbile katika maisha halisi.Yaani binadamu kwa kawaida hukua na kubadilika kitabia. Katika *Asali chungu* tunamuona mhusika Dude tangu utotoni na tunamfuata riwayani hadi anapofikia utu uzima. Mwaandishi amemkuza mhusika huyu hatua kwa hatua akieleza kila kipindi cha maisha yake kwa tafsili.

Katika riwaya ya *Anasa* mwandishi anatupa picha wazi ya kila kipindi cha maisha ya Hawa akiwa msichana mbichi, mwadilifu, mtiifu kwa mamaye hadi wakati Bw. Tamaa anayaharibu maisha yake. Baadaye anakimbilia mjini na kuanza maisha ya anasa. Kutowakuza wahusika kikamilifu ni dosari ambayo inaathiri utimilifu wa kifasihi katika riwaya. Dosari hii inanyima riwaya uchangamano.Wahusika wenye sifa ya uchangamano ndio wanasadikika zaidi katika riwaya kwa sababu ndio wanaowakilisha vizuri uchangamano wa binadamu na maisha halisi na vilevile uchangamano wa ulimwengu wanamoishi. Kukua kwa mhusika huelezea mambo mengi haswa katika jamii kwani hubadilikabadilika. Kulingana na utafiti wetu kuhusu vijana, wazazi huzidi kuwaelewa zaidi kiumri wanapokua kwani wao huwa na mabadiliko kitabia katika jamii.

### 2.2.2 Wahusika Bapa

Hawa ni wahusika ambao huumbwa maksudi na mwandishi au msanii kwa lengo fulani maalum. Wahusika bapa huwa hawabadiliki yaani wakibuniwa kama wazuri basi wanadumisha uzuri wao hadi mwisho. Wahusika hawa kwa hivyo huwa na sifa maalum (mraba mmoja) katika *Asali Chungu*, wahusika wa tabaka la kibwenyenye kama vile zuberi na Bi. Amina ni wahusika bapa, ambao wamepewa sifa maalum kuendeleza maudhui.

Wamesawiriwa kama watu wabaya ambao wanachangia sana uozo katika jamii. Anapokuwa madarakani kama disii, Bw. Zuberi anajitokeza kama mfisadi. Tunaweza sema kuwa mhusika bapa ni wa kinadharia tu au kiubunifu kwa sababu sifa hiyo ya uzuri au ubaya si ya kawaida. Aghalabu mtu huwa na tabia changamani kulingana na hali katika jamii.  Katika *Anasa*, mhusika Anasa pia ni bapa. Akiwa nyumbani anasumbua wazazi, shuleni vilevile nyanyake pamoja na walimu wamechoshwa naye na kuamua kumuita Hawa aje amchukue.  Kule mjini anaendelea na tabia mbovu na baadaye kuwa jambazi sugu. Ni vigumu kuwa na watu kama hawa katika jamii na wakiwa ni kwa unadra sana.

### 2.2.3 Wahusika Vijana

Katika utafiti wetu, tunashugulikia usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya Kiswahili. Kwa hivyo kundi hili la wahusika ni muhimu sana na lazima tuliangazie. Katika utangulizi wa utafiti wetu tulitoa fasili kadhaa za dhana ya ujana. Tulisema kuwa ujana ni kipindi kati ya utoto na utu uzima, unaelezwa kama kipindi cha maendeleo ya kimwili na kwa ukomavu na mwanzoni wa utu uzima. (Kennedy 2007) anasema kuwa kulingana na sera ya kitaifa kijana ni mtu yeyote ambaye umri wake ni baina ya miaka kumi na mitatu na mitano na ishirini na minane. Mkutano mkuu wa umoja wa mataifa (2002) unafasiri kuwa vijana ni wale watu walio kati ya umri wa miaka kumi na mitano na ishirini na minane. Kwa hivyo kwa maoni yetu, kiwango cha ujana kinatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine na tutajikita kwenye mtazamo wa sera ya kitaifa – miaka kumi na mitatu na ishirini na minane.

Tukirejelea riwaya tatu teule, wahusika vijana ni wengi - kwa mfano katika;
*Asali Chungu*: - Dude, Shemsha, Latifa, Baya, Semeni,
*Fahari ya Mateso*: Mateso na Maria
*Anasa*: Hawa, Anasa, Tineja, Daudi, Ziporah na Kalekye

Uhusika wa vijana katika riwaya hizi ni muhimu sana kwa sababu mwandishi anatathmini changamoto wanazokumbana nazo maishani. Kwa maoni yetu, tunaonelea kuwa vijana wametumika kama wahusika wa kiuamilifu kwani mwandishi amewatumia kuwasilisha lengo au shabaha yake. Hisi za mwandishi zimepitishwa kwa umma kupitia wahusika. Tukiwasawiri wahusika katika nafasi walizozichukua ndipo tunaona utendakazi wao. Licha ya kwamba wanapitia changamoto aina tofauti wanaweza kujikomboa na kufaulu maishani. Haya yatachangia tu uamuzi wao na kuchukua

mwelekeo chanya. Kwa mfano; kuachana na ulevi, wizi, uasherati, na kutia bidii katika kazi yoyote ile ambayo itamsaidia maishani. Kwa mfano: katika *Fahari ya Mateso*, kijana Mateso aliteseka mwanzoni mwa maisha yake ya utotoni lakini baadaye kutokana na bidii aliyokuwa nayo anakuwa tajiri wa kutajika. Bidii yake ilibadilisha maisha yake. Pia aliwafadhili vijana kujiunga na vyuo vya ufundi ili wapate maarifa ambayo yatawasaidia maishani.

Kwa maoni yetu, hii ni njia nzuri ya kuwasaidia vijana katika jamii kwani hujiepusha na maovu mengi kwa sababu hawana muda wa kukaa bure bila kujishughulisha na chochote. Kupitia njia hii, waliofaulu maishani kupitia mpango huu huwasaidia vijana wengine wanaokua katika jamii.

Msanii hutumia wahusika wake kubainisha fikra alizonazo kuhusu historia ya jamii ya wakati huo. Mawazo yao yanawafikisha kwenye shida, yanawatoa kijijini na kuwapeleka mjini yanabadilisha mawazo yao huzaa matendo yanayolengwa kukidhi dhamira ya mwandishi. Kwa mfano katika *Anasa* ,mhusika Hawa anakimbilia jijini ili kuepukana na aibu ya kuwa mja mzito na angali mwanafunzi. Kwa hivyo Hawa anatoka kwao mashambani ambako maisha ni ya utajiri na kwenda mjini kutesekea huko. Hayo ndiyo yanatendeka katika jamii kwani vijana hasa wasichana wanakimbilia mjini ili kutafuta namna ya kujikimu maishani na kuepuka maisha ya mashambani haswa kama wameenda kinyume na matarajio ya wazazi wao kama kupata uja uzito. Wahusika kupitia riwaya, historia ya jamii fulani huendelezwa na kujulikana na vizazi vijavyo. Kwani tamaduni za kiasili huwa hazipotei hata elimu iliyoletwa na wageni kuathiri.

Ili kujikomboa na kujinasua kutokana na minyororo ya ukandamizwaji wa kijamii wasanii (wanafasihi) wajitokeze kama watetezi wa haki na ukombozi wa vijana katika ngazi mbalimbali za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kijinsia. Mitazamo mbalimbali kuhusu taswira ya vijana ni mada ambayo waandishi wengi watazidi kuangazia na kutoa mwongozo mwafaka kwa jamii zote ili kumchukua kijana hasa wa kike kwa mtazamo chanya utakaohakikisha kuwa amepewa hadhi na haki za kibinadamu.

Vizingiti katika uhusika wa maisha ya vijana hutokea pale ambapo misingi ya utamaduni wao haueleweki. Hivyo basi huweza kutokea uamuzi fulani kuhusu vijana wa kike na kiume. Wakati mwingine huwa wamepoteza watu wengine katika jamii na wanachukuliwa kama mzigo usioweza kubebeka. Ukali wa Hawa ulizidishwa na wazo kuwa Habiba (mamake) ndiye aliyemwingiza katika janga hili. Marehemu babake angekuwa hai pengine mambo hayangemwendea vibaya hivyo. Siku zilivyoendelea kupita, ndivyo Hawa alivyoendelea kusononeka … Kila alipotoka shuleni, alijipweteka kitini … na kuvurugwa na mawazo (uk 60).

Kijana awe wa kike au kiume ni binadamu mwenye thamani ambaye ana uwezo mkuu usiodhihirika moja kwa moja. Hata hivyo, ni yeye tu ndiye wa mwisho kutiliwa maanani kuhusiana na mahitaji yake ya kimsingi na wa kwanza kunyimwa haki zake za kimsingi.Vijana hunyanyaswa kimapenzi, kubakwa, mimba za mapema kwa vijana wa kike na hata kuambukizwa ukimwi.

Dhuluma hizi mara nyingi hutendewa vijana wa kike. Hii ni kwa sababu ya utamaduni na dini ambazo zimewafunza kuwa watiifu (wanyonge), waoga (wenye haya), na wanakosa uthabiti. Pia ile hali ya jamii kudhihirisha na kukubali bila ya kunena uwezo wa wanaume na tabia yao ya kutaabisha na kudhuru wanawake. Wanapofanyiwa maovu hawachukui hatua yeyote ili waweze kutetewa kisheria. Katika *Asali Chungu* (1977), Bwana Zuberi aliyekuwa tajiri wa kutajika, anamtamani na kumnajisi Semeni ambaye alikuwa mfanyikazi wake. Semeni anaamua kutoroka kutokana na unyama aliotendewa, bila kujua ya kuwa yu mjamzito. Hana mtetezi wa kukabiliana na shida aliyoipata (uk 11).

Hali mbalimbali husababisha matatizo ya vijana wa kike na kiume. Mahitaji yao huweza kuwaweka katika ushirika wa wanaume na wanawake, ambao huweza kuwadhuru. Haja yao huwa kutimiziwa matakwa yao. Katika *Asali Chungu* (1977),

> "Utatoka katika umaskini. Utajua nini maisha ….
> Utavuliwa guo la unyonge. Utakuwa mtu,
> utakuwa mtu … ukiiwacha fursa hii,
> basi maisha yako hata hutoota, wacha kupata
> tena bahati kama hii … (Uk 88)

Dude aliishi katika mazingira ya umaskini na kisha baadaye akakutana na Bi. Amina (mkewe Zuberi) aliyetumia utajiri wake kujistarehesha na vijana wa umri wa mtoto wake. Dude anaamua kujihusisha na maisha ya anasa kutokana na maisha ya umaskini ambamo amelelewa.

Katika *Anasa* (1984), Habiba (mamake Hawa), anatumia pesa kununua mapenzi kutoka kwa Daudi ambaye ni mjakazi wake.

> "Haya baba, shika," Habiba alianza kutamka huku akiwa amemnyoshea Daudi noti. Ndarahima kama hizi utazipata wapi bure" (uk 29).

Kutokana na uhaba wa mapenzi ya mzazi kwa mwanawe, huchangia kwa kuzuka kwa tabia fulani. Ukosefu wa upendo kwa Hawa kutoka kwa mamake (Habiba), Hawa alivutiwa na ukarimu wa mzee Tamaa kwake. Kwani alipowanunulia wanawe vitabu, nguo na kuwastarehesha vivyo hivyo alimfanyia Hawa. Msaada huu ulizidi sana na baadaye kumfanya Hawa kukosa kutimiza ndoto yake maishani.

> "Hawa alishangaa kugundua kuwa mzee Tamaa alikuwa ni mzee umbo tu bali starehe zake zilikuwa za kijana …. Hakuna siri iliyotoka nje kumsababisha Hawa aanze kuonywa na kuitwa 'matatu'. (uk 53).

Hali kadhalika, ni kutokana na kutofahamu kwao na ukosefu wa mikakati ya kutetea nafsi zao ambapo wananyanyaswa. Hawa katika *Anasa* (1984) anastareheshwa na mzee Tamaa ambaye anampa mimba na kisha kumtupilia mbali. Hivyo vijana ambao hujikuta katika hali hizi hugeuka makahaba ili kulipiza kisasi. Hata wanapowapata vijana huwa hawana nafasi ya kuwalea vizuri kwani daima huwa wanatatizika ili kuyakimu maisha. Hawa anajuta baada ya kujipata ana uja uzito. Majuto ya Hawa ni kielelezo cha matatizo yanayowakumba baadhi ya vijana wa kike katika familia pindi tu binti wanapopata mimba kabla ya ndoa.Visa vya vijana wa kike kupachikwa mimba vimeongozeka kwa sababu ya mfumo wa kijamii ambao umechukua mkondo mwingine tofauti na ule wa kitamaduni.  Mfumo wa kiasili ulijikita katika taratibu za utamaduni maalum. Hungepata vijana wa kiume au wa kike wakishirikiana kimapenzi na wanaume au wanawake wanaowashunda kiumri. Jambo kama hili lingejulikana hatua ingechukuliwa ili tabia kama hii isiendelee siku za usoni.

Matokeo ya mimba ya mapema ni kuacha shule, utungwaji mimba huwa na hatari zake, kama vile vifo, kutusiwa, kulemazwa na jamii, kuwapuuza hawa mama wachanga wakiwa wazazi pekee. Hivyo wao hujitwika jukumu na gharama ya ulezi pekee yao. Katika jamii huwa na ukosefu wa haki. Katika maamuzi mengi ya kijamii hali ya kuonea na kuegemea upande mmoja. Hili ni suala ambalo linafaa liangaliwe kwa mtazamo mpya na kwa tahadhari zaidi. Maana si vyema watu wawili au makundi mawili yafanye kosa kwa kushirikiana,moja lilaumiwe na lingine lisilaumiwe. Kwa mfano Bw. Tamaa na Hawa wanashiriki ngono. Baada ya Hawa kupachikwa mimba, ikawa mwisho wa elimu yake. Bw.Tamaa hakuchukuliwa hatua yoyote akabaki akiendelea na biashara yake. Jambo hili linadhihirisha ubaguzi na upendeleo. Haya ni baadhi ya matatizo yanayowakabili baadhi ya vijana wa kike katika jamii.

Mbali na sababu zinazowafanya vijana wabaki pekee yao, wanakabiliwa na tisho na changamoto ya 'vijana pekee yao' kila mahali. Majukumu yanayozidi umri wao, hekima na pia hali yao ya kuweza kudhulumiwa kimapenzi na unyonyaji. Wazazi wa vijana hawa hulaumiana kutokana na tabia mbovu walizonazo vijana wao. Hii inatokana na kutelekezwa na wazazi wao. Inafika wakati vijana wanaaibikia tabia wanazoziona na wazazi wao.

*Asali Chungu* (1977),

> 'Matendo ya Dude na Baya hayakuwa ya maana yoyote kwao wakati ule, lakini wanapogundulikana wakicheza, wale wazee waliwakaripia sana na kuwaambia waache uafriti wao. Watoto hawakupendezwa na manyanyaso hayo. Wakihisi ……….. mbona wazee wao hawachoki kuufanya? …………… kila mmoja humgombania mwanawe kuwa siye aliyeanza (Uk 38).

### 2.2.4 Wahusika Shinda

Hawa ni wahusika wanaokosa msimamo, huyumbishwa kama upepo. Wakati mwingine ni wahusika duara wakati mwingine ni wahusika bapa. Wanapelekwa mbele kulingana na tabia pamoja na mawazo ya wahusika waliopo kwa wakati huo. kwa mfano: katika *Anasa*, Hawa akiwa nyumbani kwao na mamake anaonyesha heshima sana. Lakini barabarani akienda shule na wale wasichana wenzake tabia inabadilika wanatembea kwa jozi – msichana na mvulana. Hali hii inafanya anatumbukia pabaya na Mzee Tamaa na kuanza kubugia pombe. Wahusika shinda hupatikana katika jamii zetu, kufanya maamuzi yao huwa ni balaa na hali hii huwafanya wengine kuwafanyia uamuzi ambao wakati mwingine matokeo yake huwa mabaya.

### 2.2.5 Wahusika Wazazi

Familia ni asasi muhimu katika malezi ya wahusika vijana. Pale ambapo kuna udhabiti katika asasi hii basi vijana watapata malezi na mwongozo bora lakini pale ambapo kuna utepetevu basi majukumu muhimu yatapuuzwa na vijana hawatapata mwelekeo bora. Kimsingi familia imefungamana na asasi ya ndoa ambayo inaaminika kuasisiwa naye Mwenyezi Mungu wakati alipowaumba binadamu wa kwanza Adamu na Hawa, haya ni ya kulingana na Bibilia.

Ni katika asasi hii ya ndoa na kisha familia ambapo vijana wanatarajiwa kupata malezi yanayofaa. Malezi ni mchakato changamano sana ambao unajumuisha mambo kadha yakiwa pamoja na lishe, mavazi, makao, elimu pamoja na ushauri ambao ni mwafaka.

Katika riwaya tatu teule, wazazi wameshindwa kutimiza wajibu wao wa kutoa malezi bora na ndipo vijana wanapitia changamoto nyingi.

Katika *Anasa*, Habiba anakosa kumpa mwanawe (Hawa) mwelekeo na ushauri jinsi kijana wa kike anastahili kukua. Suala hili linamfanya Hawa kulia juu ya kifo cha babake kwani anaona kuwa angalikuwa hai, hangehangaika maishani kwani mamake hana shughuli naye. Matokeo ya matatizo anayoyapitia Hawa ni kukatiza elimu yake kwa sababu ya uja uzito na baadaye kuingilia anasa na kuwa kahaba mjini.Wazazi wanastahili kujiepusha na tabia potovu wakiwa na wanao kwani wao ndio huwa kama kioo kwao kwani wanachokifanya huigwa na wao.

Mhusika Mateso, Katika *Fahari ya Mateso* katika maisha yake ya utotoni anapokua anajililia sana. Hasa pale anapopigwa na vibaka wenzake kukosa chakula, kulala kwenye baridi na kukosa elimu. Anajiuliza alichokifanyia wazazi wake na kisha kumtelekeza. Maswali anayojiuliza hayana mtu wa kuyajibu. Katika jamii kuna baadhi ya wazazi ambao huzipa shughuli kipao mbele na kuzipa za wanao kisogo. Baadaye vijana hawa wanapofanikiwa huja na kuwaomba usaidizi. Kwa hivyo tunasema kuwa wawasaidie wanawao kwa kuwapa malezi yanayohitajika kwani katika uzee, wao ndio watakao wasaidia.

### 2.2.6 Wahusika wa Kihalisia

Hawa ni wahusika ambao wasifu wao unafanana na binadamu katika hali yake ya kawaida. Kwa hivyo kama ni kijana au vijana watende vile wale vijana wenzake. Katika

utangulizi baadhi ya sifa za ujana tulizoziangazia ni hali ya nia au tamaa ya kufanya jambo fulani, hali ya mapenzi, hali ya ujasiri juu ya upole na hamu katika maisha ya raha.

Katika *Asali Chungu*, kijana Dude na Hawa *katika Anasa*, wanaonyesha sifa hizi. Mateso pia katika *Fahari ya Mateso* hajasazwa, anaonekana akimtamani mhudumu msichana kwenye ndege. Anajipa ujasiri na kumuuliza jina lake kwa kuvutiwa na umbo lake. Wanakua wapenzi na baada ya kufunga pingu za maisha, maswala haya ya vijana husawirika katika jamii.

**2.3 Hitimisho**

Katika sura hii tumejaribu kuonyesha jinsi uainishaji na uumbaji wa wahusika unavyohusiana na vipengele vingine kama vile maudhui na dhamira katika riwaya teule. Dhamira ya kufanya hivyo ni kupima utimilifu wa kifasihi wa kila kazi ili kuweza kuamua iwapo mwandishi alikuwa akipiga hatua katika uandishi wake. Kufaulu kumechangiwa kutokana na usemi wa wahusika hawa, nafasi zao katika riwaya na kuwa kimakundi kwa mfano wahusika vijana.

Ama kwa hakika, tunaweza kuafikiana kuwa bila wahusika hakuna maudhui au dhamira kwani hawa ndio nyenzo kuu katika kuendesha gurudumu la maudhui. Kwa ujumla, dhamira na maudhui ya utafiti wetu yatawasilishwa kwa namna wahusika vijana watakavyosawiriwa katika sura inayofuata.

# SURA YA TATU

# MCHANGO WA ASASI ZA KIJAMII KATIKA MALEZI YA VIJANA KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inaangazia asasi mbalimbali zinavyochangia katika malezi ya vijana katika jamii hasa tukizingatia matini tatu teule ambazo ni *Asali Chungu* (1977), *Anasa* (1984) na *Fahari ya Mateso* (2013). Asasi hizi ni asasi ya elimu, ukosefu wa ajira, vijana na hali yao ya afya (asasi ya afya) na asasi ya ndoa. Ntsebeza (1999) anaelezea kuwa asasi ni muundo wa kijamii au shirika linalotoa huduma kwa watu katika jamii kama vile elimu, usalama, afya na kadhalika. Pia ni mbinu ya kudumisha urazini wa kijamii na ushirika unaodhibithi utendaji wa kikundi fulani cha watu katika jamii. Asasi hutambulika kwa majukumu yao ya kijamii na uwepo wao daima hueleza matendo na maisha ya kila binadamu kwa nia ya kudumisha kanuni ambazo huendeleza mienendo au silka ya binadamu.

Riwaya tatu teule ziliandikwa wakati ambapo mabadiliko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yalikuwa yanakumba jamii za Afrika Mashariki. Jamii hizi zilikuwa zinahisi athari za utandawazi. Baadhi ya asasi za kijamii ambazo zimechangai katika malezi ya vijana katika matini tatu teule ni elimu, ndoa, makazi, ukosefu wa ajira na hali ya afya miongoni mwa vijana.

### 3.1 Asasi ya Elimu

Elimu ni utaalamu wa kujiendeleza kimaarifa na kiutafiti. Elimu hudhihirika kama asasi yenye athari za kuendeleza mitagusano ya watu katika jamii kulingana na Meyer (1977). Elimu huwafanya watu wajikomboe kimawazo na kuwawezesha kujitegemea. Mfumo wowote wa elimu huchangia katika kuwapa vijana maarifa na maadili yafaayo katika jamii. Baadaye mhusika huweza kujiajiri au kuajiriwa. Elimu miongoni mwa vijana ni suala muhimu sana kwa kuwa ndilo humtoa katika hali duni ya maisha.Wao hujinyakulia nyadhifa mbalimbali serikalini na katika jamii. Mhusika Mateso katika *Fahari Ya Mateso* (2013), Mateso alianza kuona nuru ya maisha ikimwangazia nuru. Alikuwa na imani kuwa siku moja angekuwa kama watu wengine waliosoma kwa bidii na hatimaye kuajiriwa katika nyanja mbalimbali. Kulingana na ukuaji wa gharama ya maisha, umaskini na ukosefu wa vifaa muhimu baadhi ya wahusika vijana wamelazimika kuacha shule mapema. Pia masuala ya uja uzito, ukosefu wa maadili mema na maelekezo kutoka kwa wazazi na hali ya mandhari mhusika anakoishi yanachangai katika kudorora kwa elimu yao.

Vijana wanapokuwa shuleni hufanya bidii ili kuboresha maisha yao ya baadaye. Elimu huwawezesha kufahamu mambo yanayohusu nafasi katika ujumla wake. Mabadiliko yamewapa nafasi sawa kimasomo vijana wa kike na kiume. Kuna vijana wengi werevu wana nia ya kusoma lakini wazazi wao huwa hawana moyo wa kuwasadia. Wao hujali starehe zao tu na siyo ufanisi wa watoto wao maishani kupitia elimu.

Katika riwaya ya *Anasa,* Habiba mamake Hawa anamfokea anaporudi kutoka shuleni badala ya kumkaribisha kwa maneno matamu yanayomtia moyo masomoni. Jambo hili linamfanya Hawa kuanza kurudi nyumbani akiwa amechelewa na pia kuanza tabia ya kuwa na “rafiki” wa kiume kama mamake. Kwa hivyo, kupotoka kwa Hawa maishani kulitokana na mamake Habiba. Tunayaona haya katika (ukurasa wa 5-6).

> “Kisirani gani hiki huwa; huu ni wakati wa kinda kama wewe kurudi nyumbani? Baada ya kuweka mkoba wake wa vitabu juu ya meza, Hawa alianza shughuli zake.Hawa alikuwa mwanafunzi katika shule ya msingi na siku chache zilizopita alikuwa ameanza kuchelewa nje. Kila alipoulizwa alisema mwalimu wa hesabu alikuwa ametufunga…”

Vijana wanaohudhuria masomo hutumia muda wao mwingi kufikiria masomo yao. Lakini wanapokaa bure tangu jua lichomoze hadi litue hugeuka kuwa hatari. *Fahari ya Mateso* (2013)

> “Siku moja, Mateso alijifanya kana kwamba alitaka kwenda msalani kujisaidia. Ulikuwa mwendo wa saa tano asubuhi. Alipiga kona kuelekea nyuma ya jengo la madarasa huyoooooo…! Baada ya mwezi mmoja tu, alionekana mitaani akatiwa mbaroni na kurejeshwa kituoni, Dagoretti. Polisi walimvamia akinusa gundi huku akirandaranda (uk 37-39)”

Katika *Anasa (*1984),mazingira huathiri tabia za watoto. Tabia ya wizi na upekuzi wa mapipa unajawa na vijana wa mtaa wa Mahere. Vituko hivi vinaenea katika kijiji cha Mahere kwa sababu watu wazima hawawajali watoto na vijana.

> “Anasa alipendelea mchezo sana na kila wakati alionekana
> Akiwasukumasukuma wenzake .Aliogopewa na watoto ……
> uliishia vitani. (uk.99)

Elimu ni mkombozi mkubwa wa maisha ya mwanadamu na inapaswa kuwasaidia vijana kupambana na mazingira yao hatimaye yawe mahali pazuri pa kuishi. Tunaunga mkono mawazo ya Millet (1969) anasema “Elimu ni nguvu na nguvu ni elimu”. Elimu inasaidia vijana kuona uhalisia wa maisha yao kwa kujenga uhuru wa ndani, mintaarafu mwanga na maadili na utu wema. Elimu isiwe chanzo cha kuharibu tunu ya maisha bora ya jamii.

Kuna elimu ya vitabu na elimu ya maisha. Katika *Asali chungu* (1977), Shemsha amehitimu masomo yake ya utabibu na sasa anataraji kupata mchumba. Jinsi mwandishi anavyotuelezea kuwa elimu ya dunia pia ina umuhimu wake.

Mhusika kijana Shemsha anaonekana kuikosa elimu hii ya dunia kwani angefanya utafiti kuhusu maisha na ukoo wa mpenziwe Dude kwani walikuwa na uhusiano wa kijamii. Jambo hili linafanya ndoa yao kutodumu.

> "… Shemsha alikuwa ameshamaliza masomo na atafika kwao
> mnamo saa nne za asubuhi.Zuberi kila siku aliomba dua Mungu
> amjalie Shemsha amalize masomo yake ya utabibu salama usalimini. (uk.139)

> "Duu ---Duuude, nina------mama yako ali-niusia nikwambie,
> b---babako ni Bwana zuu—zuberi ----kwam-----mbia. (uk. 185)"

Riwaya ya *Anasa* (1984) Hawa anaendelea kuonyesha ushujaa mkubwa katika masomo yake. Anakuwa na bidii za kila namna. Akifanya kazi anaifanya kwa bidii zake zote. Kule nyumbani Hawa anaogopwa na vilevile kuheshimiwa. Hana dharau kwa watu wenye kujiheshimu lakini waliojaribu kumchezea aliwanyambua. Anajiheshimu, kujielewa na kujitawala. (uk.36-39)

### 3.2 Asasi ya ndoa

Ndoa ni asasi ya kibinadamu ambayo imezuka katika historia yake kama njia mojawapo ya majukumu ya kijamii. Iwapo ndoa ingeasisiwa na binadamu aina mbalimbali za ndoa zingekuwa na thamani sawa. Ndoa za wanawake wengi na wanaume wengi hunawiri katika jamii zilizoendelea kiteknolojia. Ndoa za mke na mume mmoja hudumu na ni yenye thamani kubwa kwa mujibu wa Luscombe (2010). Biblia hudhihirisha ndoa kama

asasi takatifu na iwapo binadamu wangekuwa waasisi, wangepata uhuru wa kuchagua aina ya uhusiano wa ndoa. Haya ni mawazo ya mtaalamu Bacchiocchi (1974).

Wanawake wakomavu wanaridhika kuwanasa vijana wa kiume kama walivyo wanaume wakomavu ambao hujivunia vijana wa kike. Mwanamke anayehusika katika kumteka kijana wa kiume huwa hatilii maanani ushauri wowote. Wanawake wakomavu huwa na mbinu za kuwanasa hawa vijana wa kiume kama wafanyavyo vijana wa kike; wanapoolewa na wanaume wakomavu. Wanawake hawa huwa wapishi stadi na kila wakati huwastarehesha hawa vijana wa kiume. Hutuzwa, hufurahishwa na kupewa starehe ambazo vijana wa kike wa rika lao hawawezi kuwafanyia. *Anasa* (1984) Habiba ambaye mumewe alikuwa ameaga dunia anaonekana kuanza kujistarehesha na vijana wadogo wa kiume.

> "Habiba alianza kuwatupiatupia vijana macho. Aliwatania, akasimama nao na hata kuwaalika kwake nyumbani"(uk.8).

Kwa maoni yangu,wanaume na wanawake ambao hushiriki uasherati na vijana wa rika la wana wao wanastahili kuchukuliwa hatua kali. Kwa sababu vijana hawa wanaishia kutotimiza ndoto zao maishani pia kuambukizwa maradhi kama ukimwi ambayo hayana tiba.

Wazazi walio na maono huchangia sana katika elimu ya watoto wao, kwani watoto hawa huwa tegemeo la wazazi wao na hata jamii. Kwa ujumla, wazazi hujitolea kutoa rasilimali muhimu kwa minajili ya kuwaelimisha watoto wao.Tumaini la wazazi huwa kuwa watakuwa walezi wao baadaye. *Anasa* (1984), Habiba anaonelea kuwa elimu ya

mwanawe Hawa ndiyo itakayowasaidia maishani hasa atakapopata kazi nzuri. Kwa hivyo, Hawa alipokuwa shuleni alipewa zawadi ainati ili atie bidii zaidi.

> “Habiba alimtunukia zawadi ya baiskeli kwa kazi yake nzuri naye aliendelea kuwarushia vumbi wanafunzi wenzake”. (uk. 37)

Zuberi katika *Asali chungu* (1977), anaomba Mungu amjalie awe hai mpaka atakapomwoza mwanawe Shemsha mume, halafu tena ikiwa Mungu atataka achukue roho yake, achukue baada ya miaka mitano. Anazungumzia haya baada ya Shemsha kukamilisha masomo yake ya utabibu ili pia awe na fahari juu ya bintiye. Ombi la mzazi yeyote yule kwa mwanawe ni kuona amepiga hatua kimaisha ili awe na maisha mema na pia amsaidie wakati atakapozoeka.

> ---Huondoki mpaka nikupakulie chakula, wakati mwingine alikesha huko na jimbi lilipowika alielekea nyumbani huku akipiga mluzi kama mvivu. (uk 3-5).

> “Habiba alikuwa tayari kuutumia uwezo wake kumlainisha Daudi kama siagi. Aliuingiza mkono wake ndani ya sidiria ----“haya baba shika, Habiba alianza kutamka akiwa amemnyoshea Daudi noti.” (uk 28-29)

Hili tendo ni kinyume cha matarajio ya jamii za kiafrika na hata jamii nyinginezo ambazo huthamini maadili ya kijamii. Hali hiyo huonekana kama ukosefu wa maadili.

De Beavoir (1985) anasema “Asasi ya ndoa imempa mwanamke majukumu mawili muhimu, kwanza ni kuzaa watoto na pili ni kuhakikisha kuwa anatimiza mahitaji ya kimapenzi kwa mumewe na kuangalia nyumba yake. Lakini Bi. Amina katika *Asali Chugu* anaenda kinyume na haya ambapo mwishowe ndoa za watoto wake zinaishia babaya. Bi. Amina na Shemsha bintiye wanabadilishana mpenzi mmoja ambaye ni Dude. Baadaye inatambulika kuwa alikuwa nduguye. Bi Amina anapoona kuwa mumewe

Zuberi amezoeka na kuanza kuugua, anakata kauli ya kuanza kuwatafuta watoto wa umri wa wanawe. Anakutana na kijana wa kiume Dude na kuanza urafiki wa kimapenzi naye. Starehe za pesa na safari zikawa kwa wingi.

> “Amina aliseme hivyo hivyo huku akipachika mkono wake na kulaza kichwa chake begani pa Dude. Sema kama unanipenda Nasema kwamba nakupenda. Mara elfu na moja, Dude alijibu huku anacheka…Dude aliwaza jana alikuwa wapi, leo yuko wapi na kesho atakuwa vipi?  (uk. 109)

Dude anaonelea kuwa maisha yake yanabadilika kutoka katika hali ya umaskini na sasa yumo katika tabaka la juu (utajiri). Kuna uwezekano kuwa tendo kama hili limetokana na hali ya utambulisho miongoni mwa vijana wa kiume na kike. Hata hivyo, kujihusisha nalo kunazua mitafaruku kati ya vijana na wazee, viongozi na hata mazingira. Sosholojia ya Fasihi inaeleza kuwa tofauti zinazojitokeza katika maisha ni muhimu ili kuelewa mfumo mzima wa maisha na namna ambavyo mfumo huo huchangia katika malezi ya vijana. Suala la umaskini pia limechangia vijana kutafuta wanawake wanaowazidi kwa umri ili kujipatia hela za kujimudu katika maisha. Kina mama nao wameamua kuwa wakiwa na pesa wanapata njia rahisi ya kuwanasa vijana ili wazishughulikie haja zao za mwili.

Mfumo wa kiasili ulijikita katika taratibu za tamaduni maalum. Hungepata vijana wakishirikiana kimapenzi na wanaume au wanawake wanaowashinda kiumri hatua ingechukuliwa kwa wahusika hawa ili tabia kama hii isiendelee siku za usoni. Lakini majilio ya wakoloni pamoja na wageni wengine kutoka nchi za kimagharibi ulivuruga hali hii. Mtagusano wa wageni hawa ulivuruga utaratibu wa mifano ya ulezi ambayo ilikuwako. Elimu ya kimagharibi ilileta mambo mapya na hata kuvuruga thamani pamoja na maadili katika jamii.

Kiwango cha masomo si hoja mradi awe mtulivu, mwaninifu na mpole. Elimu siyo mume au mke. Mwandishi amethibitisha haya kupitia kwa Shemsha katika *Asali Chungu* (1977). Shemsha amehitimu kama tabibu na walichumbiana na Dude ambapo siku anayorudi anamjulisha babake (Zuberi) kuwa Dude ni mpenzi wake. Licha ya kwamba Dude hana kisomo lakini hulka zake zinamfurahisha Zuberi ambaye yuko tayari kuzinunua kwa pesa.

> "Nimefurahi na kurejea kwenu pamoja, wewe shemsha mwanangu, na Dude ni mwanangu pia, nimevutiwa na kuwa na mapenzi naye. Leo Mungu ameteremsha rehema zake. Mmekutana wenyewe, mmetakana wenyewe, mmekubaliana wenyewe, mimi sina pingamizi. (uk. 142)

Mila na desturi za jana zinafaa zife kwa utundu wake wa kukataa kuzipasha mila za leo kulingana na vijana hawa zinawaruhusu kujichagulia kuingia au kutoingia katika ndoa, kuchagua mchumba na kuendelea na elimu kadri ya uwezo wake.Vijana wanastahili kujichagulia wapenzi wao hasa wanapofika umri wao. Jambo la wazazi kuwaamulia lilipitwa na wakati. Ikiwa shida yoyote itampata kijana akiwa kwenye ndoa ile, hatakuwa na wakulaumu.

Katika *Fahari ya Mateso* (2013) kijana Mateso, baada ya kupitia milima na mabonde maishani, baadaye anamuoa Mwanaheri ambaye ana kisomo kinyume na Mateso. Maisha yao yanakuwa ya baraka na ufanisi.

> "Mwanaheri hakuhitaji ujuzi zaidi katika kazi yake mpya ya ukurugenzi. Alikuwa amepata ujuzi wa kutosha katika chuo cha kitaifa cha mafunzo alikojipatia stashahada ya kiwango cha juu… (uk. 159).

Uhusiano wa karibu wa vijana wa kike na kiume ambao hawajaolewa huweza kuleta mtafaruku au mazoea fulani miongoni mwao. Ikiwa wazazi hawana shughuli na urafiki wao, mambo huweza kwenda mrama. Kwa hivyo ni jambo la busara wazazi au mzazi

kujua rafiki au marafiki wa mwanao na kuwa na mazungumzo miongoni mwao kuhusiana na maisha. Katika jamii pale ambapo kuna uthabiti katika asasi ya ndoa, vijana watapata maelezo na mwongozo bora lakini pale ambapo kuna utepetevu basi majukumu muhimu yatapuuzwa na vijana hawatapata mwelekeo bora. Vijana wa kiume huanza kuwa na hisia za kimapenzi kwa vijana wa kike marafiki wao. Chanzo cha haya ni mazoea kati ya wahusika hawa. Hushirikiana kwa kila jambo kama ndugu; hutembeleana na hata huweza kubadilishana zawadi wakati wa sherehe fulani.

Ukosefu wa uwajibikaji miongoni mwa mmoja wa wazazi au wazazi wote unaweza kuathiri sana hali ya vijana hao. Kwa mfano mzazi yule anabeba jukumu la kukidhi mahitaji ya familia anayapuuza majukumu yake kwa kuingilia ulevi na ukware basi familia itaumia sana kwa sababu mbali na kushindwa kugharamia mahitaji ya kimsingi kama chakula, anashindwa kulipa karo na hivyo kuvuruga elimu ya mwanao. Dude katika *Asali Chungu*, alilazimika kuacha shule kwa kulemewa na changamoto kama hizi.

*Asali Chungu* (1977) vijana hawa Dude wa kiume na Baya wa kike, wazazi wao walikuwa marafiki, lakini hawakuyajali malezi ya watoto wao.

> "…mwishowe akaelewa vyema kuwa mmoja kati ya wawili aliowaona huwa mwanamke, na wa pili mwanamume, mara nyingi alivutwa na kuhusudi vitimbi vyao. Siku moja akajaribu na kunipenda… Baya akawa mwanamke, naye mwanaume. Hawakuwa na uhuru kama wazee wao. Ilibidi waibeibe… wale wazee waliwakaribia na kuwaambia waache uafriti wao….. Siku wanaokamatwa, huwa ugomvi mkubwa baina ya wazazi wao. Kila mmoja hugombania mwanawe kuwa siye aliyeanza." (uk. 37-38)

Uhusiano mwingine wa kimapenzi baina ya vijana ni kati ya mhusika Hawa na Daudi katika riwaya ya *Anasa* (1984). Haya yanajielezea zaidi kupitia kwa barua ambayo Hawa alimwandikia Daudi katika (uk.21). Vijana walifunzwa maadili katika jamii katika

mambo ya kimapenzi, vijana walionywa dhidi ya kujiingiza katika visa vya ngono. Kuporomoka kwa kiwango cha maadili katika jamii kumesababishwa na mambo mengi; kwa mfano, kuporomoka kwa mifumo ya utamaduni katika mipangilio ya familia kumechangia hali hii. Zamani, watu waliishi vijijini kama familia moja ambapo vijana wangepata ushauri kutoka kwa wazazi wao. Hali hii imebadilika kwa sababu vijana wanapata nafasi ndogo ya kukaa na wazazi wao ili washauriwe.

Hali ya kukosa utulivu katika ndoa au kifo huwafanya vijana wa kiume na kike kujichanganya maishani kwa sababu ya kukosa wasia ufaao kutoka kwa mzazi au wazazi. Hali hii huwafanya vijana kuacha shule, kupata uja uzito, kuingilia ulevi miongoni mwa changamoto zingine maishani. Huwazuia kuwania ndoto zao maishani. Katika *Fahari Ya Mateso* (2013), mtafaruku kati ya Bw. Matasi na Bi. Riziki katika ndoa yao, ndio sababu kuu ya  Mateso kuteseka. Baadhi ya mateso haya ni; ukosefu wa elimu, kurandaranda mitaani, wizi pamoja na ulaji wa vyakula mapipani. Mateso haya yanamfanya kijana Mateso kufikiria zaidi kuhusu walipo wazazi wake, anatamani kuwajua kwani wangemsaidia katika hali ile. Anawaza na kujiuliza maswali.

> “Jambo gani nililowakosea wazazi wangu hadi wakanitelekeza jinsi hii? Mama yangu ni nani na anaishi wapi? Mbona hawezi kukumbuk… ni kosa ngai nililotenda hadi nikaachwa katika msitu huu uliojaa simba, fisi, chui, mbogo… (uk. 25).

Vilevile katika *Anasa* (1984) Hawa anajililia kuwa kifo cha babake kimemwathiri maishani, kwani anaona hatapiga hatua kielimu. Hili ni kutokana na mienendo ya mamake, Habiba kuingiliana na Daudi kimapenzi. Kila mzazi ana wajibu wa kuhakikisha kuwa anamwelekeza mwanawe kwa kila njia.

> “ukali wa Hawa ulizidishwa na wazo kuwa Habiba ndiye aliyemwingiza katika janga hili, kama angejibeba kama mwanamke anayejiheshimu mambo haya pengine yasingalitokea.kama babake marehemu angekuwa hai pengine mambo hayangemwendea vibaya hivyo (uk. 60)

Maisha ya ndoa pia huimarika tu iwapo vijana wa jinsia zote watalelewa katika mazingira yenye usawa. Hili linapokosekana wao hulaumiana. *Asali chungu* (1977) Bi Amina na Zuberi hawajabarikiwa kupata mwana wa kiume. Suala hili linaleta shida hasa atakayeirithi mali yao ni nani? Wamefuata tamaduni za kiafrika kuwa wana wa kike huwa hawarithi mali bali wa kiume tu. Ingawa Bi Amina na Zuberi wana mali na wana wa kike wawili bado wanajililia kutopata mwana wa kiume.

> "Zuberi alisema kwa sauti iliyoroa machozi na huzuni.
> 'Unaelewa jinsi nilivyokuwa nikitamani tupate mtoto wa kiume, lakini vipi"(uk.102)

Waandishi, kupitia kwa vijana wa kike na wa kiume wamepambanua namna ambayo wahusika hawaelewi athari za kushiriki katika mapenzi yasiokuwa na maana ya dhati.Vijana wote huathirika kwa njia moja au nyingine. Wanapojikuta matatani ndipo hutambua kuwa walifanya maamuzi mabaya. Uhusiano wa kimapenzi kati ya vijana wanaowazidi kiumri ulibainisha ukosefu wa maadili. Kama tulivyosema hapo awali msichana kupata mimba nje ya ndoa katika maisha ya kitamaduni ilikuwa ni muhali sana.

Hali hii huwaletea majuto kwani huwa ni jukumu la mzazi au wazazi kuandama mienendo ya vijana wao na kuwashauri vilivyo la sivyo, vijana wao hupotoka njia. Mfano katika *Anasa* (1984) Hawa anajikuta katika hali tatanishi hasa baada ya kupokea aina aina ya zawadi kutoka kwa Bw.Tamaa zikiwemo pia starehe. Mwishowe, anajipata mja mzito na kuacha shule. Inabidi akimbilie mjini na kuingilia maisha maovu ya kuzurura zurura ovyovyo mitaani pamoja na ulevi.

> "Anasa za sinema, madansi na viburudisho kem kem vilikoma
> na badala yake simanzi ukiwa na wasiwasi ukachukua mahali pake. (uk. 60).

Asasi ya ndoa imedhihirika kuwa na athari nyingine ambazo ni chanya na pia hasi. Hatua yoyote ambayo mtu ameamua kuchukua ni lazima iwe na manufaa au hasara kwa mtu binafsi, familia na jamii. Sheria, mila na desturi inaruhusu kila jamii ifanye juhudi kuhakikisha ya kwamba miundo misingi ya kijamii ni thabiti ili kuleta mshikamano wa familia na taifa. Mshikamano wa kitaifa ni muhimu na iwapo familia haziwezi kuhakikishiwa usalama, ukuaji na maendeleo husambaratika.
Ukosefu wa usalama nyumbani utazifanya familia nyingi kutengana naye Njagi (2011) katika jarida lake kuhusu familia anafafanua kuwa familia zilizo na mzazi mmoja ni zile ambazo mzazi huyo huchukua majukumu ya kuwakuza watoto peke yake. Kuna aina mbili za familia zenye mzazi mmoja, zile ambazo kwa wakati fulani zilikuwa na wanandoa na zile ambazo mtu hajawahi kushiriki ndoa tangu kuzaliwa.

Familia za mzazi mmoja huweza kusababishwa na mambo mengi yakiwemo talaka, kifo, kutengana, kifungo cha maisha, ugonjwa na kususia familia. Njagi anatamatisha kwa kusema kuwa mzazi akiwa peke yake hukumbana na changamoto nyingi kama vile jukumu la kuwalea watoto peke yake, upungufu wa fedha za kuyakimu mahitaji, kuwapa watoto ambao wameanza kubalehe nidhamu, usumbufu kutoka kwa mashemeji, upweke kutuhumiwa na watu juu ya swala la maadili, watoto hukua kwa kumfahamu mzazi mmoja na upungufu wa mawasiliano baina ya watoto kadri wanavyokua. Maswala haya yote yanaangaziwa katika jamii, yasipo angaziwa kwa jicho pevu huleta athari mbaya kwa familia, jamii na nchi.

### 3.3 Malezi na afya miongoni mwa vijana (Asasi ya afya)

Masuala ya afya katika jamii hushughulikia utunzaji wa afya ya watu katika jamii. Hayaangazii wagonjwa tu bali pia hushughulikiwa wale ambao wana afya njema ili wazidi kuimarisha afya yao. Ni dhana yenye ujumbe kuhusu namna ya kutunza mwili na kuepuka ndwele (Wijayaratne, 2011).

Nchi yoyote inayoendelea hutegemea watoto wenye afya njema ambao hukua vijana na baadaye katika utu uzima huchangia katika maendeleo maishani mwao. Kuzorota kwa afya ya vijana huwafanya wanyonge na wanaotegemea jamii ili kujinusuru katika maisha yao. Hali hii inaeleweka mno kupitia fasihi katika fikira na usemi wa vijana.

*Asali Chungu* (1977), Dude alijitosa katika ulevi na uvutaji sigara. Starehe hizi zinamfanya ajiunge na kikundi ambacho kinamwelekeza pabaya. Anajiingiza katika anasa ambazo zinamkanganya maishani na kuwa na mwisho mbaya maishaini. Ulevi husababishwa na ile hali ya mtu kupata uraibu wa pombe. Ulevi huathiri hisia za mtumiaji mpaka akajisahau, asielewe alifanyalo.

Ukosefu wa ajira huchangia vijana kujihusisha na ulevi. Ili kujiondoshea mawazo mengi kuhusiana na matatizo ya kiuchumi yanayowakabili katika jamii. Wengine husema kuwa ulevi huwasaidia kuzisahau shida zinazowakumba. Katika ukurasa wa 126, Baya alikuwa mtoto mdogo juzi, leo hatamaniki. Kakubuhu kama kizee cha miaka mia–mkofu dhaifu wa hali na sura uso umekwabuka, mdomo umebambuka, mwili umefusikafusika kwa sababu ya ulevi. Baadhi ya vileo huathiri vijana sana kiafya hivi kwamba utamuona

kijana wa umri mdogo wa miaka ishirini na mitano anayeonekana mkongwe zaidi kuliko ule umri wake. Hali ya afya ya vijana iliyodhoofika huwakosesha washirika wao furaha. Mtu yeyote anayehusiana na washirika hao hugundua kuwa kuna jambo linalowazonga.

Mateso katika *Fahari ya Mateso,* wanapoyazuru majalala hawana utambuzi wala ubaguzi wa mabaki ya vyakula au matunda, wanakula wanachokipata katika hali inayopatikana kiwe kizuri au kibovu. Hali hii ya randaranda mitaani inamwingiza Mateso katika kikundi cha vibaka wanyang'anyi wanaowaibia watu pesa, rununu na vibeti. Haya yote yanasababishwa na hali ya njaa miongoni mwao. Changamoto za kiafya wakati mwingine hazitokani na afya ya vijana wenyewe bali pia ya wazazi wao.

Baadhi ya watu hufikiri kuwa afadhali vijana waishi mashambani kwa sababu maisha ya mijini huwashajiisha kujitia maisha ya anasa na hivyo kukumbwa na hatari. Haya ndiyo mawazo ya Hawa, kwani tabia za mwanawe Anasa zilikuwa zimemchosha.

> "Katika siku zake za kwanza, alikuwa hawajui watoto wa
> kijiji hicho na alibaki pekee.Kulikuwa hakuna mapipa ya kuchokora
> na pia hapakuwa na vichorochoro vya kufanyia maovu.Tabia yake
> alianza kuwa nzuri kwani mazingira ya shamba yalikuwa tofauti na ya mjini.
> Alikuwa katika ulinzi wa nyanyake" (Anasa, uk.106)

Vijana wana upungufu, hawajihusishi katika shughuli muhimu zinazoweza kuwapunguzia hatari zinazotokona na hali yao ya afya. Huhusika katika matendo yanayohatarisha maisha yao, hutumiwa kama kigezo cha kuthibitisha wasiwasi walionao watu wazima kuwahusu vijana. Vijana wanabainika kama wahusika ambao hawawezi kujidhibiti na hali hii. Huwafanya washiriki matendo ambayo huzorotesha hali yao ya kiafya. Katika *Anasa,* ukurasa wa (87-88) watu wengi wanampigania Hawa, jambo

ambalo linamfurahisha sana kwani anajinyakulia mafungu zaidi ya wenzake.Tabia ya Hawa inabadilika kutoka msichana aliyejiamini, kujilinda na kuvitawala vitendo vyake na kuwa msichana wa kuyatoa matusi, kutembea ovyo na kuziweka pesa mbele ya utu wake. Anaanza kunywa pombe kama komba. Anaweza kumeza tangi zima na kubaki imara daima kama mnara wa kanisa.

### 3.4 Makazi yanavyoathiri vijana

Historia ya makazi ya umma huonyesha kuwa ukosefu wa makazi miongoni mwa vijana ambao hawajaoa hudhihirika kama tatizo kubwa kwa waathiriwa. Haya ni maoni ya Hopper (2010) ambaye alifanya utafiti kuhusu wanaume wanaokosa makazi. Anatoa hoja kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya ajira na makazi. Hili ni dhihirisho kuwa ukosefu wa makazi au makazi duni hutokana na matatizo ya kiuchumi.

Makazi yanayofaa huwafanya vijana wajihisi kama viumbe muhimu katika jamii. Ni njia mojawapo inayowapa tumaini na kutenda mambo ambayo yataimarisha maisha yao kibinafsi na ya jamii kwa ujumla. Shemsha katika *Asali chungu*, wanaishi maisha ya utajiri, baada ya masomo yake anahitimu kama mwuuguzi na kuwafanya wazazi wake kujivunia.

Riwaya tatu teule zinabainisha kuwa baadhi ya vijana huishi katika makazi yenye hali za kusikitisha. Katika *Fahari ya Mateso*, Mateso baada ya kutelekezwa na wazaziwe, baadaye anajipata akirandaranda barabarani na chokoraa wengine.

> “Makazi yao yalikuwa popote pale Walipopatwa na giza jijini
> nyakati za jioni.Vitanda vyao vilikuwa sakafu ya veranda.”(uk 18)

Pia kule wazazi wa Mateso wanakoishi, Mathare, hali ya maisha ni duni. Chumba kile kimoja ndicho cha malazi, sebule na meko mumo humo. Kuna makochi mawili ya sifungo yaliyorarukararuka na kutengeneza makao safi ya panya na mende (uk. 3). Hali hii ya maisha ndiyo pia inayowachangia wazazi wale kushindwa kumtunza mwanawao na baadaye kumtelekeza.

Vijana wengi ambao wanakaa bure bila kazi huwa na ushawishi wa kujiingiza katika uhalifu ili wajipatie riziki yao ya kila siku. Ukosefu wa ajira ni tatizo nyeti sana miongoni mwa vijana. Vijana ambao wamepoteza matumaini ni tishio kubwa kwa usalama wa nchi. vijana wanaohamia mijini kwa minajili ya kutafuta riziki huishi katika makazi yasiyoridhisha kutokana na ukosefu wa mapato. Mara ya kwanza Hawa kwenda mjini, anaelekea kwake Kalekye. Katika kijiji cha Mahere, mahali ambapo kila mtu hakujalishwa na chochote. Katikati ya nyumba hizi takataka zilitawanyika kila mahali. Uchafu na vinyesi vilitawanyika kila mahali. Vijumba vya makaratasi vilisongamana kama viota vya mizingi.(uk 82-83). Mandhari haya yanaonyesha kuwa mahali pale kuwa makazi yale ni duni. Haya yanatokana na ukosefu wa mapato. Hawa anatorokea mjini kwa sababu ya uja uzito. Anatafuta njia ya kujikimu maishaini.

Maisha ya vijana yanapoongoka na kuimarika kiuchumi, wao hupenda kuishi mahali penye hadhi! Baada ya mhusika Mateso kupitia panda shuka kadhaa maishani, anagundua kipawa chake katika riadha kinachomsaidia kupiga hatua maishani. Katika *Fahari ya Mateso,*

> "Jumba la mateso huko kitengela lilimgharimu takriban shilingi
> milioni kumi na mbili na laki saba.Jumba lenyewe lilikuwa la
> kifahari na bila ubishani lilihitaji mwanamwari wa kuishi ndani---(uk 79)

Hali ya sasa ni tofauti na ya kale, ambapo katika utamaduni wa kiafrika walionavyo huwashirikisha wasionavyo katika jamii husika. Hili limeletwa na suala la utabaka katika jamii. Ufanisi wa mtu mmoja katika jamii katika hali ya ukale, ulikuwa ufanisi wa jamii nzima. Mabadiliko kihistoria, kijamii na kiutamaduni yamezua ubinafsi kiasi kwamba waajiri wana makazi yao maalum mbali na wanakoishi maskini.

Utabaka ni hali inayojitokeza katika jamii ambapo watu hujigawa kulingana na mali waliyonayo, elimu, madaraka kazini au imani na dini. Kujigawa huko ndiko hujitokeza kama utabaka. Kati ya matabaka mengi yanayoshuhudiwa katika jamii, tabaka la walalaheri na walalahoi ndilo linaloshamiri sana ikawa tajiri na maskini ni kama maji na mafuta yasiyoingiana

Suala la utabaka limekita mizizi miongoni mwa jamii nyingi za kibinadamu. Ni suala la kiasili katika maisha ya kibinadamu japo wakati huu linaonekana kuwa changamoto kwa sababu ya itikadi na mitazamo ya watu kulingana na hadhi zao. Coser (1963) kama anavyomnukuu Honore de Balzac (1799-1850) na kuelezea kuwa:

> "Ukiwa na familia ambazo hazina uwezo unaolingana kimaisha
> katika sehemu yeyote ile, utaona utabaka ukijitokeza"

Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi itatusaidia kuchunguza masuala kama haya jinsi yanavyoiathiri mifumo mbalimbali ya kijamii ambayo ndio chanzo cha kuwepo fasihi. Katika *Asali Chungu*, jamii ya Mzee Zuberi na mkewe Amina, ni walalakheri nayo ile ya kina Dude ni walalahoi.Tunayaona haya kutokana na maisha wanayoishi.

> "Dude aliranda ili kutafuta kazi, lakini siku zilizofuatia alizurura tu.Kukosa
> kazi kulikuwa kwingi kuliko kupata; na hata kama kijana mmoja alipata,
> ilikuwa kazi ya kuosha vyombo, kupika au kufagiafagia kwa wahindi; (uk. 65).

Kila asubuhi, vijana hawa hurauka wakiwa na matumaini ya kupata ajira lakini ni wachache tu wanaochaguliwa na wahindi hao. Wengi hubaki katika hali ya kukata tama.

Malipo ambayo wanapewa baada ya kazi za sulubu za mchana kutwa ni ya kusikitisha vilevile ni kama hali ya utumwa.

Naye Zuberi katika ule upande mwingine alikuwa amewaajiri wafanyikazi kwenye 'kasiri' yake. Makazi huwafunza vijana wa kiume na kike mambo mengi hata wale ambao hawakufikiri kuwa wangeingia maisha ya wizi na ukahaba ambao ni wa ufiski wa izara, maisha ya kutumika kama tambara bovu la kufuta uchafu wa watu usiowajua na wasiojali huwatisha.

Elizabeth (2006) anaelezea kuwa tatizo la makazi hutokana na hali ya kiuchumi na elimu. Hili limetokana na ukuruba na jamii za mitaa kama vile Mathare. Maendeleo na ukuaji wa jamii huenda pamoja na ongezeko la idadi ya watu. Hali hii husababisha msongamano wa watu kutoka mitaa inayokaliwa na idadi kubwa ya watu. Katika *Anasa*, mhusika Anasa anajifunza wizi kutokana na vijana wa pale Mahere, hasa waliokuwa wakubwa kwake.Wanawatatiza watu kwa kuwapora simu na hata vibeti vyao mchana. Pia Hawa anapofika kijijini Mahere, anakaribishwa kwa tabia (ukahaba) ya wasichana wa pale na Kalekye.

> "Alipozungumza na rafikiye Kalekye, alionywa kuwa hakuwa
> tofauti na wasichana wale wengine ambao waliiweka miili yao
> tayari kwa aliyetaka kuishikashika.Kuona hasira zake hazingemfaa
> kwa chochote, alijitolea kuwamtumishi bora ijapokuwa hakuwa akipendelea
> kuchezewa. (uk.86).

Katika hali kama hiyo ya ongezeko la idadi ya watu, ambayo husababisha msongamano wa watu mijini, mitaa ya madongoporomoko huzaliwa kama vile Mahere kwa akina Mateso. Matokeo ya hali hii ni kwamba vijana huingilia unywaji wa pombe haramu na vileo vingine hatimaye kutumbukia katika uhalifu.

Changamoto wanazopitia vijana wa kike kama vile uja uzito unachangia wao kujitosa katika tabia ambazo zinachangia uozo katika jamii. Wao huwa na mahitaji mengi ambayo huchangia wao kutafuta msaidizi kwa kujiingiza katika usherati ambao huwaletea magonjwa yasiyo na tiba kama ukimwi

**3.5 Ukosefu wa ajira**

Ukosefu wa ajira ni miongoni mwa matatizo makubwa sana yanayowakumba vijana. Hali hii ndiyo inayosababisha kuongezeka kwa uhalifu.Vijana wengi sana ambao wanakaa bure bila kazi huwa na ushawishi wa kujiingiza katika uhalifu ili wajipatie riziki yao kila siku. Ajira huwa na azma ya kuwasaidia wakazi wa eneo fulani kuendeleza jamii, kujitosheleza na ustawi wa mtu binafsi. Huwezesha watu kuimarisha uwezo wao kiuchumi kwa njia ya mipango na huduma. Gidden (1990) anasema kuwa kuna haja ya kuwepo kwa ajira ili iweze kusaidia na kuafikia malengo yake sana kuwanufaisha wanajamii. Hali hii itakuwa kama kichapuzi katika maendeleo ya asasi nyinginezo kwa mujibu wa Charlene (2012).

Ukuaji wa uchumi, haujaruhusu uwepo wa nafasi za ajira kwa vijana wenye umri mdogo. Ni asilimia ndogo tu ambayo hubahatika kuajiriwa, wengine hubeba mzigo mzito wa kukosa ajira hasa wanapokamilisha maovu mengine ya kijamii kama vile matumizi ya mihadarati na ukahaba. Katika *Anasa*, Hawa, baada ya kutambua kuwa ni mjamzito, anaacha shule na kutorokea mjini ili kutafuta njia ya kujimudu maishaini. Sheria za ajira na haki za watoto zingefuatwa, hangeweza kuajiriwa kwenye baa na kutumika na

wanaume kama kifaa cha kuwafurahisha. Alikuwa mdogo kwa umri kuifanya kazi ile (uk. 82-86).

Wanawake waajiri basi huweza kuwarai vijana wa kiume waajiriwe na kuwaweka katika mtego wa mapenzi. Hali hii ni njia ya kusawazisha mapenzi wasiyopata katika ndoa. Katik*a Asali chungu* Bi Amina mkewe Zuberi, anaamua kutafuta kijana barobaro ambaye angemkamilisha haja yake katika ndoa. Bi Amina anamfahamisha Bw. Zuberi kuwa Dude angekuwa mfanyikazi wao pale nyumbani. Kwani ana tabia njema kumbe kuna mpango mwingine juu ya Dude.

> "Mbona umesimama?Mbona unasita?pitapita---Njoo
> Bwa-mdogo;au unaona haya?Amina alikuwa na ulegevu
> wote wa kike macho yake, midomo yake,mikono yake-----Haya
> yote yalimwakinishwa Dude kuwa hakuwepo mwingine aliyeitiwa
> dhaifa ile ila yeye." (uk. 95).

Vijana walioelimika si lazima waajiriwe wanapokamilisha masomo yao. Wakipewa mtaji wanaweza kuendeleza biashara yao na hatimaye kusaidia vijana wengine kupata maarifa na nafasi za kazi. Katika *Fahari ya Mateso*, kijana Mateso, anafaulu katika riadha kutokana na bidii aliyokuwa nayo na baadaye kuazisha mradi ambao unawasaidia watu.

> "---Walikubaliana kuwa na vitegauchumi kadhaa na ndipo wakaanzisha
> biashara ya cyber café mjini Kitengela----.biashara ya cyber café ilinawiri
> mno na baada ya miezi minne tu wakaanzisha kampuni ya usafirishaji ya
> MARISOLO TOURS"(Uk 158).

Bidii ni muhimu ili kijana yeyote yule afaulu katika lile analotenda katika jamii. Ni vyema kujali muda wa utendaji kazi. Hapaswi kujihusisha katika mambo ya starehe huku akitarajiwa kuwa kazi wakati mwingine. Huhitajika kufanya kazi bila kupumzika almuradi ajikimu maishani.

Hitimisho kwa ukosefu wa ajira upo katika kuwapa vijana mafunzo ya kuwawezesha kujiajiri wenyewe na hivyo hata kuweza kubuni nafasi za ajira kwa wengine badala ya kazi zile ambazo zinawaacha wasomi kwa kazi za kujiajiri afisini kwa kazi kama hizo hazipo.

### 3.6 Mahitimisho

Tatizo kubwa ni kuwa vijana haawafikii asasi nzuri za ushauri. Asasi zenyewe zinapaswa kuwafunza vijana kuhusu uhalisia wa maisha. Iwapo asasi mbalimali zikiwatambua vijana basi zitakuwa zenye manufaa kwa vijana ambao watakuwa wenye manufaa kwa jamii zao. Lazima vijana wafanye jitihada ili waendeleze maisha. Kupotoka kwa vijana ni kupotoka kwa jamii nzima. Vijana wamekuzwa ili kudhihirisha umuhimu wa mabadiliko chanya miongoni mwao ili wawe wenye manufaa kwao wenyewe na katika jamii wanamoishi.

# SURA YA NNE

# MAUDHUI NA UTAMBULISHO WA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA ASALI CHUNGU, FAHARI YA MATESO NA ANASA

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tutaangazia utambulisho wa wahusika vijana katika jamii ya waandishi wa riwaya teule kupitia kwa maudhui. Maudhui ni mafundisho yenye umuhimu fulani yanayowasilishwa kupitia kazi za kifasihi. Mwandishi hutumia “nyenzo”au “fani” ili kufikia lengo hili. Tutashughulikia maudhui na utambulisho wa vijana kupitia kwa mandhari, wahusika na matumizi ya lugha katika matini tatu teule.

Maudhui makuu ambayo waandishi waliyaangazia ni ya kijamii hasa kuhusu maswala ya taswira na mitazamo tofauti tofauti. Mazrui na Syambo (1992) wanadai kuwa mtunzi wa riwaya kwa mfano, ana njia nyingi za kueleza lolote analotaka kutueleza. Tunaunga mkono mawazo yao kwani waandishi wa riwaya teule wametumia njia anuwai kuwasawiri na kuwatambulisha vijana katika jamii yao.

## 4.1 Wahusika katika ujenzi wa maudhui na utambulisho wa vijana

Tulieleza hapo awali kuwa wahusika ni wale watu au vitu vinavyosababisha matukio fulani kutokea au kutendeka. Msokile (1993) ametubainishia wahusika kama vitu, wanyama au watu katika kazi ya sanaa. Pia mimea, mashetani na mazimwi inaweza kuchukua nafasi ya wahusika. Katika matini tatu teule, waandishi wamewaumba wahusika wao kwa lengo la kufanikisha maudhui yao.Wameangazia changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo vijana katika jamii.

### 4.1.1 Dhuluma na Unyanyaswaji wa vijana

Kwa kuwarejelea vijana hii ni hali ya kuwanyima haki yao ya kibinadamu kama elimu, huduma za afya pamoja na huduma za jamii. Swala la unyanyaswaji linazingatiwa katika misingi ya kitabaka. Kila mara kuna hali mbili katika jambo hili. Upande wa kwanza ni wa watu wenye uwezo, wenye mali, wanaomiliki nyezo na njia kuu za uzalishaji mali. Upande wa pili ni wa wale wasiokuwa na chochote, binadamu wanaonyonywa nguvu na jasho lao.

Maudhui haya yanaendelezwa na mhusika Mateso katika *Fahari ya Mateso* anapotelekezwa na wazazi wake na kuokotwa na wasamaria wema. Anapelekwa katika makao ya wana wakiwa ambapo baadaye anatorokea mjini kwa sababu ya shida kuzidi. Alirandaranda barabarani na vibaka wengine. Kupata chakula ilikuwa shida hakuwa na wa kumjali.Tunadhihirisha kwa kupitia haya;

> "Maisha ya kijana huyu yalijaa na kujaza mapaku mapaku
> pamwe na madoa doa ya madhila na makuruhu, usumbufu, lawama
> na laana mzomzo. (uk. 14)

Dondoo hili linaonyesha kwamba mhusika Mateso anajitambulisha kama mnyonge na mkosa haki kwani hakuna anayemjali katika jamii ili kuokoa maisha yake. Vijana ambao hujipata kwa hali kama hii huathiriwa kisaikolojia na hata kuweza kumsukuma katika tabia zingine mbovu ambazo hazifai. Vilevile kuna tatizo la kujitambua ambapo kijana wa aina hiyo hataweza kujitambua ipasavyo, hasa kuhusiana na wazazi wake pale anapoulizwa na wenzake.

### 4.1.2 Madhara ya ulevi

Swala la ulevi limechangia katika ukosefu wa maadili mema miongoni mwa vijana. Mhusika Dude katika *Asali Chungu* anajitosa katika tabia ya ulevi inayomwelekeza kuwa na mpenzi wa kike ambaye anamshinda mbali kiumri. Jambo hili linamfanya kutojielewa.

> "… akatoa chupa ya wiski, akatoa gilasi, akafunga mlango wa friji,
> aelekea chumbani kwake. kile kilikuwa kitu pekee kitakachomsaidia yeye kuwaza
> alilotaka kuwaza, au kusahau alilotaka kusahau Wiski ndio kitu pekee (uk. 130).

Vijana wametambulishwa kama walevi. Hali hii imechangiwa na hali ya mazingira wanakokulia.Vijana wa jinsia zote wameathirika na ulevi. Katika jamii ya waandishi wa riwaya tatu teule. Hawa, katika *Anasa* anajitosa katika ulevi baada ya Bw. Tamaa kumdanganya kwa pesa na zawadi nyinginezo ili afaulu katika njama zake. (uk 46-47).

Vijana wengi wameathirika na ulevi kwa sababu ya athari za makundi fulani katika jamii. Iwapo vijana wazembe wanakuwa na mtagusano na wenzao ambao tayari wana uraibu wa ulevi wanaweza kushinikizwa kulewa.Wengine hulewa ili kupata ujasiri wa kuwawezesha kushiriki katika uhalifu bila woga kama vile Hawa na Mzee Tamaa katika *Anasa*.

### 4.1.3 Ujasiri kama wasifu wa vijana

Vijana hujiamini kuwa wanaweza kupambana na hali fulani katika jamii.Wao huamua na kutorudi nyuma katika ndoto zao. Hukabiliwa na changamoto zinazoweza kuibuka katika harakati za kujiendeleza aidha kazini au nyumbani.Wao hutumia uwezo, ukakamavu na udhabiti kama mizani ya kuwapimia.

Kupitia kwa vijana, waandishi wa riwaya za *Anasa*, *Asali Chungu* na *Fahari ya Mateso*, wamewachora baadhi yao kuwa wa kijasiri katika jamii ili kupambana na milima na mabonde katika jamii. Katika *Asali Chungu*, Dude ana huruma na wema wa roho yake. Dude alimchukua Baya aliyekuwa ameloa damu na kumpeleka hospitalini hata baada ya kukatazwa na "bosi" wake Bi. Amina. Hiki ni kitendo cha kijasiri kinachotokea na imani ya roho yake.

Katika *Anasa*, Hawa anajitosa uwanjani kwa kuwa na mpenzi mmoja na mamaye.  Hawa anaonyesha ujasiri bila woga (uk. 24-25) Kupitia haya, tunaona kuwa kijana wa jinsia ya kike anatumika kama chombo cha starehe. Tayari Daudi ashamaliza masomo yake ya sekondari lakini anataka kumharibia Hawa, aliye katika shule ya msingi. Baadaye, Daudi anaonekana akiwahepa Hawa na mamake Habiba. Hawa, anaonyesha ujasiri kwa kuwa na mpenzi mmoja na mamake. Daudi pia anaonyesha ujasiri kwa kuwatumia kwa pamoja Habiba na mwanawe Hawa. Katika jamii jambo hili huwa kinyume cha utamanduni  na huchangia hata laana kwa kizazi fulani ambao hujuta baadaye.

### 4.1.4 Elimu

Vijana wanachukulia kuwa elimu na ajira kama nguzo muhimu katika ukombozi wao. Maoni haya yamechochewa na utambuzi wa mchango wa elimu kuwafahamisha kuhusu haki zao kama binadamu wenye uwezo na haki sawa.Vile vile elimu itawawezesha kusomea taaluma nzuri zitakazowapatia  kazi zenye kipato kizuri. Aidha hii itakuwa mbinu ya kujikuza kiuchumi na kuepukana na tabia ya utegemezi ambayo ndiyo inayowapelekea kuteseka.

Waandishi wameonekana kuwachora wahusika vijana wakitafuta maarifa shuleni katika *Asali Chungu* Shemsha amesoma mpaka akahitimu kama tabibu.

> "…Shemsha alikuwa ameshamaliza masomo yake ya utabibu…. (uk. 139).

Hawa pia katika *Anasa* anaonekana akisoma. Baadaye, Anasa ambaye ni mwanawe anapelekwa shule ili kujipatia elimu. Kupitia wahusika vijana, waandishi katika riwaye teule wamehusisha jinsia zote kike na kiume kujishughulisha na masomo. Mashirika mawili ya UNICEF na UNESCO (2002) yanaelezea kuwa mgogoro wa kiuchumi duniani na mizozo ya vita vinafifiza juhudi za elimu miongoni mwa watoto na vijana. Hali ya uchumi, siasa, zikiwemo dhuluma miongoni mwa watoto na vijana limechangia katika kukatiza elimu yao hasa wa kike.

Mhusika Hawa katitka *Anasa* anakatiza masomo yake kwa sababu ya uja uzito. Yule aliyechangia katika kukatizwa kwa masomo yake Bw. Tamaa hachukuliwi hatua ya kuwajibikia hali ya Hawa baadaye. Kwa kumrudisha shuleni aendelee na masomo yake. Haki inakosa kutendeka kati ya jinsia hizi mbili. Mara nyingi mtoto au kijana wa jinsia ya kike anapopata uja uzito, hukatiza masomo yake na wengi wao huteseka maishani, nao wale wa jinsia ya kiume waliochangia katika hali ile huendelea na masomo yao.

### 4.2 Mbinu za lugha na utambulisho wa vijana

Hizi ni mbinu watumiazo wasanii wa fasihi ili kutia nguvu maana ya maudhui wanayoyasanii. Pia huwa zinatumika kama njia za kueleza jambo kwa undani na ubunifu zaidi na isiyowezekana katika lugha moja kwa moja. Matumizi ya mbinu za lugha

yametumiwa na waandishi wa riwaya za *Asali Chungu*, *Anasa* na *Fahari ya Mateso* kwa kuendeleza maudhui. Baadhi za mbinu za lugha zilizotumika ni:-

### 4.2.1 Majazi

Matamuzi ya majazi tulivyosema hapo awali yanashabihiana na sifa za mhusika fulani. Ukimpa mhusika jina la kimajazi basi unawajibika kuhakikisha kwamba unamhusisha mhusika huyo ili atende vitendo au aseme mambo ambayo yanashabihiana na jina lake.

Baadhi ya wataalam wakiwemo wafula (1999), Njogu na Chimerah (1999) na Wamitila (2003) wanaelezea kuwa mbinu ya kimajazi hutumiwa na waandishi kuwapa wahusika majina yanayomwelekeza msomaji kwenye wasifu wa tabia zao. Mbinu hii humsaidia msomaji kuelewa tabia ya mhusika anayezungumziwa kwa urahisi. Katika *Fahari ya Mateso*, kuna mhusika kijana anayeitwa Mateso. Jina hili lina maana ya kuteseka katika ukuaji wake tunamuona akitelekezwa na wazazi, anahangaika kama chokoraa barabarani jijini Nairobi. Mateso ni mhusika anayewakilisha vijana kutoka jamii au tabaka maskini hasa mwanzoni mwa riwaya. Mhusika huyu anaendeleza maudhui ya umaskini na mateso.

Umaskini katika taifa hupimwa kulingana na uwezo wa kifedha na hasa kiasi cha matumizi ya wastani ili kupimia kiwango cha mapato. Kulingana na viwango vya kimataifa, iwapo familia haina uwezo wa kugharamia matumizi ya dola moja kwa siku basi familia kama hiyo ni maskini. Umaskini unasababishwa na ugavi mbaya wa rasilimali za katika jamii ambao hauna usawa.Watu wachache wanamiliki mamilioni na mamilioni ya ekari za mashamba huku wengine wakiwa hawana hata nukta ya ekari.

Katika *Asali Chungu*, kuna majina ambayo yametumika kimajazi. Baadhi ya majina hayo ni kama vile Dude, ambaye ni mwanawe Semeni aliyekuwa mfanyakazi wa Zuberi. Semeni amempatia mwanawe jina hili kutokana na misukosuko anayokumbana nayo maishani kama kumbukumbu ya hali hiyo mbali na kuwa jina linalomtambulisha mhuskia huyo.

> "Hapo Baya huwa mke, na Dude huwa mume. Na siku nyingine na nyingine tena, huowana na kuowa na bila ya kikomo. Tena Baya humfundisha Dude yale aliyoyaona kwa mamake na mtu wake wapo kitandani pao." (uk 37).

Kutokana na maelezo haya, jina Baya, ingawa linamtambulisha mhusika fulani, pia linatoa maelezo murwa kuhusu matendo ya mhusika huyu ambayo ni mabaya kama jina lake. Matendo ambayo ameyarithi kutoka kwa mama yake. Mhusika Baya anaendeleza maudhui ya ubaya katika mapenzi na usherati. Katika jamii vijana huwa hawaruhusiwi kujihusisha na maswala ya ngono kama hawajahitimu umri fulani. Lakini Baya anaonekana kujihusisha na shughuli hizi mapema.

### 4.2.2 Taswira

Taswira ni kinga ya utunzi ambapo lugha inatumiwa kusawiri picha fulani kutokana na maelezo yanayotumia maneno mateule au tamathali za usemi. Mbatiah (2001) anasema kuwa kupitia kwa njia hii mtunzi anamwezesha msomaji kuona, kuhisi au kunusa kitu kinachoelezwa. Madhumuni huwa ni kuziamsha hisia zinazoshughulikiwa .Yaani mwandishi anajaribu kuziteka hisia fulani za msomaji. Haya hutendeka ili maudhui yanayoshughulikiwa yapate undani na uhalisi unaokubalika. Taswira huwa za aina mbalimbali ; mathalani taswira za uoni , usikizi , hisia n.k. Katika *Asali Chungu*,mwandishi anaelezea haya kitaswira.

> "Zuberi angalipita moja kwa moja kama si jicho lake kuanguaka juu ya mlango wa kutokea ukumbini…Hakujua kwa nini alivutiwa na picha ile kwa maana hakuwa na kituo cha kutajamali uzuri wowote… kichaka kizuri chenye vituo na miti mikinda Kwa mbali kuna maporomoko ya maji kwenye kilima. Kwa mbele, gogo bovu limelala. Mbwa mwitu wa kijivujivu kainama anang'wafua windo lake la sungura-kesha linyofoa pande moja damu mbichi inatiririka na nyingine imetapakaa kwenye majani (u.k 8)

Katika kifungu hiki tunafasiri kuwa mwandishi ametumia picha ya kichaka kizuri chenye miti mikinda kwa maana Semeni ambaye ni msichana mrembo na bado kigori, nalo gogo bovu ambalo limelala mbele ya milima limetumika kwa maana ya Zuberi, Mzee aliye mtovu wa maadili ambaye anawinda Semeni jinsi mbwa mwitu awindavyo sungura. Mwandishi ametumia mbwa mwitu amwindavyo sungura.

Mwandishi ametumia mbwa mwitu kumrejelea Zuberi na sungura kumrejelea Semeni. Ile damu mbichi ambayo imetapakaa kwenye majani ni ile damu ambayo humtoka msichana aliye bikira akiingiliwa na mwanaume kwa mara ya kwanza au mwanamke yeyote akibakwa. Kifungu hiki kinaelezea kuhusu uhusiano baina ya wanaume na wahusika vijana wa kike na jinsi baadhi ya wanaume wanavyowadharau vijana wa kike na kuwachukulia kama vyombo vya kuwafurahisha. Mapenzi miongoni mwa wazee wa kiume na vijana wa kike imekita mizizi na jambo hili ni kinyume cha matarajio katika jamii.

### 4.2.3 Matumizi ya Tashbihi

Mbinu hii pia huitwa tashbiha. Hutumika kulinganisha vitu viwili kwa kutumia maneno kama, "mithili ya", "kama", "ja" n.k. Ifuatayo ni mifano ya matumizi ya mbinu hii katika riwaya ya *Asali Chungu*;

> Mazingira yake ya mwanzo yalikuwa kama wingu kubwa lililomkalia Dude. Lilimwinamia kwa uzito wote, asiweze kuinua macho na kuangalia upande wa pili wa ulimwengu wake. Kule ambako angeliweza kuona upeo wa hulka njema, hakuuona. Badala yake lilimgubika katika mazingira ya upotofu na laana (uk-88).

Katika kifungu hiki, wingu kubwa lililomkalia Dude lina maana ya hali ya umaskini na usherati wa mamake, alimozaliwa na kukulia, hali ambayo ilimfumba macho asiweze kutafuta riziki yake kwa njia nzuri. Nalo wingu lililomgubika katika mazingira ya upotofu na laana, ni kwamba alichukuliwa na Amina mkewe babake awe akimtimizia mahitaji ya kimwili huku naye akitimiziwa mahitaji ya kifedha. Katika *Anasa*, tunamuona Bw. Tamaa akiendeleza tabia yake ya kimapenzi na vijana wadogo.

> "Mzee Tamaa alipohakikisha kuwa Hawa amelainika kama mkate wa bofulo uliochovywa chaini, alianza kumwekea Hawa chambo baada ya chambo"(uk.47)

Kutokana na maelezo haya, kwa sababu ya kuzama katika mapenzi zaidi, mwili wa Hawa unalinganishwa na mkate ambao umepakwa siagi ambao huwa umelainika na kutafunwa kwa urahisi bila kuhangaika. Kupita hali hii Hawa anapotelewa na fahamu na Bw.Tamaa anapata fursa ya kushiriki ngono naye. Bw.Tamaa na Hawa wamechorwa kama walevi na washerati. Katika jamii watoto na vijana wadogo huwa hawaruhusiwi kujishughulisha na ulevi.Wale ambao hujishughulisha na ulevi hutazamwa kama wapotevu katika jamii. Katika *Fahari ya Mateso*, mhusika mtoto Mateso anaonekana kuwa na tabia ya wizi baada ya kutembea na kuishi na wale vibaka wenzake katika barabara za mji wa Nairobi.

> "Upesi kama umeme, Mateso alinyakua mkoba wa mama huyo chwaap! Mithili ya kipanga anayehisi njaa anavyomnyakua kifaranga wa kuku"(uk 30).

Kutokana na dhiki ambayo Mateso anapitia maishani, inambidi atafute njia ambayo itamsaidia kumaliza matatizo yake. Ndipo anaingilia wizi ili aweze kupata angalau chakula kwani njaa ilimzidi. Mateso anaendeleza maudhui ya wizi.Tabia ya wizi hurudisha nyuma maendeleo katika jamii na mara nyingi vijana hukatazwa kujihusisha na tabia hii.Wale huziba sikio na kuendelea nayo huishia pabaya kwa kuumizwa na hata kuuawa.

### 4.2.4 Methali

Methali ni kauli fupi iliyosheheni maana na ujumbe na inachukuliwa na jamii kuwa kiwakilishi cha hekima na busara. Methali huwa na sehemu ya turathi za kimapokeo za jamii zinazobeba falsafa, mila, miiko and desturi za jamii (Mbatiah 2001). Methali zina umuhimu mkubwa kisanaa katika kutajirisha maudhui na fani ya kazi ya fasihi. Katika kazi nyingi za fasihi, methali zimetumika kujenga uhalisi wa mandhari na wa utamaduni na jamii zinazohusika. Kutokana na maelezo haya methali basi inafafanua maudhui kupitia maana ya ujumbe ibebayo. Katika *Fahari ya Mateso*, Mateso anaonekana mwenye bidii sana katika riadha. Kila mashindano walioshiriki alihakikisha kuwa amejipatia tuzo.

> "Mateso alipoitwa mbele ya gwaride, makofi yalipigwa kwa wingi huku wanahabari wakisukumanasukumana. Kila mmoja aliwania kumpiku mwengizwe kupata picha na maelezo Mwafaku kutoka kwa kijana huyo. Chanda chema huvikwa pete nalo jina jema hung'aa gizani. (uk 50).

Kutokana na nukuu hili, maudhui ya ushindi na bidii yanaendelezwa na mhusika Mateso. Kutokana na maana ya jina lake (Mateso) hakufikiri kuwa siku moja angetamanika na kufuatwa na watu kutokana na bidii yake. Hawa anaonekana ameshaathirika na zile

zawadi Bw. Tamaa alikuwa akimpa ili kumvuta karibu naye. Safari zao za kwenda Thika zilizidi ili kujistarehesha. Dondoo hili linatueleza zaidi.

> "…walimpiga Zipora chenga mara kwa mara ili wawe na uhuru wa kutosha. Kwa kweli mchovya asali hachovyi mara moja." (uk. 53).

Maudhui ya mapenzi yanaendelezwa kupitia methali hiyo, kwani ilikuwa mazoea kwao kwenda kujistarehesha. Umaskini pia ulichangia katika tabia hii kwani Hawa hakuwa na mzazi wa kumpa pesa na zawadi zingine alizozipata kutoka kwa Bwana Tamaa.

Maudhui ya laana yanaendelezwa na Dude katika *Asali Chungu*. Tangu kuzaliwa kwake amekuwa na mikosi ambayo imemwandama maishani.

> "…upeo wa matendo yake ulikuewa mkubwa, na kila siku ulizidi kurefuka. Hakujua aanze wapi kuyafikiri matendo hayo. Kweli hukuna msiba usiokuwa na mwenzake. Dude amefikiwa na misiba si haba. (uk 57).

Mamake Dude, Semeni, alimpa mwanawe jina hilo kutokana na misukosuko anayokumbana nayo maishani kama kumbukumbu ya hali hiyo. Dude pia anajipata katika makazi yake walikoishi na mamake mlezi (Bi. Pili) ambaye alikuwa dadake mamake (Semeni). Dude walijamiiana na Baya (Mwanawe Bi. Pili) ambaye alikuwa ndugu naye.

Katika utamaduni wa kiafrika kitendo hiki huwa cha laana kwa watu wa ukoo mmoja. Pia baadaye anamwoa Shemsha, bintiye Zuberi ambaye ni babake Dude. Baadaye pia anampachika dadake Shemsha (Latifa) uja uzito. Katika hiyo familia moja, Dude ni mpenzi na mamake shemsha na Latifa Bi. Amina ambaye ni mke wa Bw. Zuberi. Kwa hivyo, damu ya laana inaonekana ikimfuata Dude maishani, anajaribu kuwazia chimbuko

la dhiki anazopitia maishani. Kauli hii inatupa funzo kuwa katika jamii tabia na matendo ya mtu huwa na athari fulani.

### 4.2.5 Maswali ya Balagha

Hii ni mbinu ambayo hujitokeza katika fasihi pale ambapo mtunzi au mhusika huitumia kwa lengo la kumtanabalisha msomaji au msikilizaji, anauliza maswali bila majibu. Dhima ya maswali ya balagha ni kutoa mawazo au hisi za ndani za mhusika au kuweka jambo fulani wazi kwa hadhira na ambalo linahitaji kuangaziwa nao kwa makini. Aidha, maswali ya balagha hutumiwa kusisitiza wazo ambalo mwandishi hakudhamiria kulieleza tu au kulitaja bayana. Katika *Anas*a, maswali ya balagaha yametumika kwa mfano:

> …Bi. Kizee alimgeukia tineja huku akisema unataka nikupofushe kwa
>
> kuona uchi wa nyanyako ndio uniheshimu? "Nyanya alifoka. "Toa –aaaa toa__ Hahahaaa unadhani nimeona uchi wavinyanya wangapi na macho mawili imara daima? ----toa uangalie kama nitayafumba macho." (uk 76)

Maudhui ya nidhamu au maadili yanaendelezwa na maswali haya ya balagha. Tineja anaonekana akibishana na mama mzee; haonyeshi heshima kwa nyanya. Ukosefu wa maadili mema miongoni mwa watoto na vijana katika jamii, kumechangia jamii kuendeleza vizazi ambavyo vimejiingiza katika wizi, ulevi, usherati na tabia zingine mbaya zisizofaa. Hamna heshima miongioni mwa wazee kwa vijana na watoto. Jamii ambayo huonyesha utovu wa nidhamu, huwa imejaa maovu mengi ambayo hutendeka. Kuporomoka kwa kiwango cha maadili katika jamii kimesababisha na mambo mengi. Kwa mfano, kuporomoka kwa mifumo ya utamaduni katika mipangilio ya familia kumechangia hali hii.Vijana wanapata nafasi ndogo ya kukaa na wazazi wao ili washauriwe.

Katika *Fahari ya Mateso*, Mateso alijiuliza msururu wa maswali kwani hakuwa anaamini kama anaweza kufanya jambo maishani kionekane kuwa kimetoka kwake.

> "Wakati mwingine, mapenzi ya machoni chimbuko lake moyoni na rohoni; moyo ukipenda hutuma hisia machoni… Lakini msichani mrembo kama huyo angekubali kijitu ovyo kama mimi? Kijitu kisichokwisha kuharibiwa miguu kwa kutafunwa na funza vile? Kijitu lilicho na makovu ya majerahaa ya siku za mwambo? (uk. 121).

Mateso anajiuliza maswali kama mrembo yule atamkubali kama mpenziwe, lakini bado anapiga moyo konde, hajiamini, anajidharau. Katika jamii mtu hujidhalilisha kuwa hawezi jambo fulani kwa sababu ya woga na kuitupa bahati yake maishani. Maswali anayojiuliza Mateso yanadhihirisha kuwa hajiamini kama anaweza kufanya jambo lolote, amejidunisha yeye mwenyewe kupitia kwa hali yake ya maisha hapo awali.

### 4.2.6 Mandhari na ujenzi wa maudhui katika malezi na utambulisho wa vijana

Mandhari huwa ni kipengele muhimu katika uchanganuzi wa maudhui. Mandhari ni mazingira ya utendaji au usimulizi. Njogu na Chimerah (1999) wanafasili mandhari kama mahali maalum yaliyojengwa na mtunzi na ambapo wahusika hukaa na kuingiliana na hivyo kuzua matukio ya kiutendaji. Naye Wamitila (2008) anasema kuwa mandhari si mazingira ya kijiografia tu bali hurejelea maswala mengine kama vile kipindi cha matukio au mawanda wa matukio kama inavyodhihirishwa na matendo ya wahusika. Mandhari katika riwaya hufungamanishwa na wahusika, matumizi yao ya lugha, matendo yao; usawiri wao wa mwandishi pamoja na hulka zao katika kukuza na kuendeleza maudhui.

Katika riwaya tatu teule (*Asali Chungu*, *Anasa* na *Fahari ya Mateso*), mandhari ni ya kiyakinifu kwani mazingira yanayorejelewa yanaakisi mazingira ya kawaida katika jamii

tunamoishi ambavyo ni mandhari ya kijiografia na ya kijamii. Mwanzoni mwa riwaya ya *Anasa* mwandishi amechora mandhari ya familia ya Habiba ifuatavyo.

> "Familia ya Habiba ilikuwa na mali ya kutosha. Ilikuwa baina ya familia zilizosifika kwa ukwasi katika kijiji cha Makuthuni. Walikuwa na shamba kubwa liliojaa matunda chekwa, mafenesi, machungwa, matofaa, mapera na hata mapaipai.walikuwa na ng'ombe wa kutosha na hata mbuzi. Mungu alikuwa amewatunukia watoto wawili, wa kike na wa kiume." (uk 2)

Mandhari haya yanaendeleza maudhui ya utajiri kwa akina Hawa. Mandhari haya ni ya kijamii (shamba, mimea na wanyama) yanaashiria pia uendelezaji wa ukulima katika jamii ambao unachangia katika maendeleo ya kuimarisha uchumi katika jamii. Mtaani Mahere, pale Kalekye, Hawa na Anasa waliishi, mwandishi anatupa taswira hii:

> "…vijumba vya makaratasi vilivyosongamana, kama viota vya mizingi….vilikuwa na matundu makumbwa….takataka zilitawanyika kila mahali. Vinyesi na uchafu vilivyochanginyika vilitawanyika kila mahali (uk 82).

Mandhari haya yanaonyesha kuwa watu wa tabaka la chini (maskini) ndio waliishi katika kijiji kile. Katika jamii kuna makundi ya matabaka kulinganina na uwezo wa mtu katika jamii yeyote ile. Katika *Asali Chungu*, tunaelezewa kuhusu safari za Dude na Amina wake ambazo pia zinatupa mandhari mbalimbali.

> "Amina na Dude wake waliondoka kisiwani Weba mnamo saa moja Unusu za usiku.Kulikuwa giza, kwani mwezi ulikuwa bado haujachomoza. (uk. 123).

Katika nukuu hili, tunaelezewa kuwa wakati walipokuwa wanasafiri ilikuwa usiku. Mara nyingi wanaonekana kufanya mambo yao katika giza. Waliogopa mazungumzo ya watu katika jamii kuhusu mapenzi yao, kwani yalikuwa na doa. Kwani wahusika wote (Amina na Dude) wameamua kwenda kinyume na maadili ya jamii.Wanashindana mbali kiumri,

ni kama mtu na mwanawe. Jambo hili linaashiria jinsi jamii imekuwa na uozo kimaadili. Kwa mukhutasari, Katika Sura hii tumetumia wahusika, mbinu za lugha na mandhari katika kuchanganua maudhui yaliyotupa taswira na utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule.

# SURA YA TANO

# MUKHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Tulichagua na kuchanganua riwaya tatu ambazo ni *Asali Chungu, Anasa* na *Fahari ya Mateso* kwa kuangazia usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana. Ili kuafikia malengo yetu ilitubidi kudurusu na kusoma matini teule ambazo zilituwezesha kufikia hatua hii kwa kuongozwa na madhumuni , maswali ya utafiti na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi.

## 5.1 Mukhtasari

Msukumo wa kazi hii ulitokana na tatizo la utafiti kuhusu masuala nyeti ya kijamii kuhusiana na malezi ya vijana inayopatikana katika riwaya tatu teule. Inabainika kuwa changamoto zinazokumba vijana katika jamii za waandishi wa riwaya hizi, zinafanana licha ya kuandikwa vipindi tofauti na waandishi tofauti.

Sisi tulitumia nadhiria ya Sosholojia ya Fasihi kama dira iliyotuongoza katika utafiti wetu. Tulishugulikia vipengele zifuatavyo katika kila sura vilivyotusaidia kushughulika mada yetu. Sura ya kwanza tuliangazia dhana ya ujana ilivyofafanuliwa na watafiti kadhaa, malengo ya utafiti wetu, mapitio ya mada teule, nadharia ya utafiti iliyotuongoza katika utafiti na baadaye, tukashughulikia mbinu mbalimbali za utafiti na uchanganuzi wa data husika.

Katika sura ya pili tulishughulikia dhana ya wahusika na uhusika wa vijana, uumbaji na uainishaji wa wahusika tukitoa mifano katika riwaya tatu teule. Katika sura ya tatu tumechanganua data ambayo tumeikusanya kutoka kwa riwaya za *Asali Chungu*, *Anasa*, na *Fahari ya Mateso*. Tulishughulikia mchango wa asasi za kijamii unavyoathiri malezi ya vijana.

Sura ya nne tumeshughulikia maudhui na utambulisho wa vijana katika riwaya tatu teule. Vipengele vilivyotuongoza katika kushughulikia maudhui ni uhusika wa wahusika, matumizi ya mbinu za lugha na usawiri wa mandhari katika malezi ya vijana. Sura ya tano inahusu muhtasari, hitimisho la kazi nzima, matokeo na mapendekezo ya masuala ambayo yanaweza kushughulikiwa katika tafiti zitakazofanywa katika siku za usoni.

## 5.2 Matokeo

Madhumuni na maswali yetu ya utafiti yalituongoza katika utafiti na matokeo kadhaa yalibainika. Matatizo ya kijamii na kiuchumi yanachangia pakubwa changamoto miongoni mwa vijana. Kwa mfano: ulevi, ukosefu wa maadili katika jamii, ukosefu wa ajira miongoni mwa mengine. Pia imedhihirika kuwa asasi za kijamii zimelegeza kamba katika utaratibu wa kuwaumba vijana walio waadilifu. Hali hii imechangiwa na mitagusano miongoni mwao na mandhari wanamokaa. Majilio ya wakoloni na wageni wa kimagharibi yalileta elimu ambayo imewakengeusha vijana na kubadili mtazamo wao katika maisha. Maadili yamezorota na kuchangia maovu mengi katika jamii kama ulevi, wizi, usherati, ndoa za mapema na kukatizwa kwa elimu miongoni mwa vijana.

## 5.3 Mapendekezo

Ili utafiti wowote uweze kuwa wa manufaa kwa jamii ni lazima mtafiti aweze kutambua mwanya ambao utahitaji kuzibwa na watafiti wa baadaye kwa muktadha huu tunatoa mapendekezo yafuatayo kwa watafiti wa baadaye. Katika kazi hii tumejikita katika utanzu wa riwaya, uhakiki wa baadaye unaweza kufanyiwa tamthilia. Changamoto zinazowakumba vijana katika jamii zetu zinaweza kupata suluhu ya kudumu? Mada tuliyoishughulikia itafitiwe kwa kutumia nadharia na fani zingine za kimtindo.

## MAREJELEO


Annan, K. (2001). Briefing Papers for Students "We the People's". The role of the United Nations in the Twenty First Century. InThe Millenium Report, United Nations, New York.

Bellamy, C. (2002). The State of the World's Children and Youth 2002, UNICEF and UNESCO.

Beavoir, S. (1949). *The Second Sex.* London : Campbell publishers.

Charlene, T. (2012). A Lost Generation: Youth Identity And State Decay in West Africa, Richard Weiber and Terence, Ranger eds. Post colonial Identities in Africa. London, Zed Book.

Coser, L. (1963). *Sociology Through Literature*: An Introductory Reader. Prentice Hall, Englewood Cliffs.

De Boek, F. (1999). Domesticating Diamonds and Dollars: Identity, Expenditure, and Sharing in Southern Zaire (1984 – 1997) pp 177 – 209.

Hopper, K. (2010). Public Shelter as a Hybrid Institution: Homeless Men in Historical Perspectives. The Society for The Psychological Study Of Social Science.

Kamunde, E.M. (1983). "Kilio cha Wanyonge katika Riwaya za S.A. Mohamed" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. "Tasnifu ambayo Haijachapishwa".

Kasante.D. (2001). *Popularising Gender. A Case Study of Makerere University*. A Paper Commissioned by Forum for African Literature Bureau.

King'ala, M. Yusuf (1984). *Anasa*. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.

Kimani na Njogu (1986). Falsafa ya Shabaan Robert katika Riwaya Zake Katika'MWAMKO'Jarida la CHAKINA (imehaririwa na mwandishi mwenyewe) Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kimani, N na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi,* Nairobi: J.K.F

Kiango, S. (1992). Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia za Kiswahili za Kenya. UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Katola, N. (2006). Swala la Udhalimu Dhidi ya Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili. UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Luscombe, B. (2010). Who Needs Marriage? A Changing Institution. Time press, Australia.

Mbatiah, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*: Nairobi: Standard Textbooks Graphic and Publishing.

Mbatiah, A.M (1988). S.A Mohamed kama Mwalimu wa Jamii" Tasnifu ya B.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohammed, S.A. (1977). *Asali Chungu*. East African Educational Publishers. Nairobi, Kenya.

Mogambi K. (1983). Uhakiki wa Hali ya Wanyonge katika Riwaya Tatu za S.A. Mohammed. UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi: East African Educational Publishers.

Mtua, J. (2007). Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu Ukombozi wa Mwanamke katika Tamthilia Tatu za Kiswahili. UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Muindi, A. (1990). "Usawiri wa Wahusika Makahaba katika Riwaya za S.A. Mohammed". Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Nkonge, G. (2006). Athari za Udhanaishi katika *Kichwa Maji* na *Nguvu ya Sala*. UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Nalika, *R. (2012*), Uhakiki wa Hali ya Vijana katika Riwaya ya Vipanya vya Maabara UoN Tasnifu ambayo Haijachapishwa.

Narizvi, S. (1982). *The Sociology of the Literature of Politics;* Australia, Edamund Burke.

Ntsebeza, I. (1993). Youth in Urban Africa Townships, 1945-1992”A case study of London Townships, M.A. Thesis ,University University of Natal. Department of Economic History.

Oyoo, J.S. (2013). *Fahari ya Mateso*.Wasta. Nairobi, Kenya.

Robert, K. (2007). Family Strength and Challenges In Kenya, New York, The Harworth Press

Wamalwa, D.N. (2013). Uchanganuzi wa Changamoto za Ujana katika Riwaya za John Habwe  Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Maseno. Tasnifu ambayo haijachapishwa.

Wamitila , K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi*; Nairobi; Focus Books.

Wamitila .K.W. (2008). *Uhakiki wa Fasihi; Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi; Vide-Muwa Publishers Limited.

Wijayaratne, S. (2011). Faces of Angels: Real Stores of AIDS-Affected Children in the Kibera Slums: Johns Hopkins University.